# Nipashe

Jumamosi Septemba 16, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581435

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS. 1,152,911,993

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## MAUAJI DADA WA BILIONEA MSUYA

**Mfanyakazi** wa ndani adai kuahidiwa mil. 50/-

UK. 4




UKURASA 11

KUKATIKA UMEME

# Kilio kila kona

• **Wananchi** wadai kupata hasara, TANESCO yaeleza sababu...*Uk. 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### WADAU DEMOKRASIA WATAKA MGOMBEA BINAFSI



BAADHI ya wadau wa demokrasia wameeleza matamanio yao ya kutaka kuwapo kwa mgombea binafsi na kuweka usawa wa kijinsia kwenye...

UKURASA WA 5

### AJALI HIACE ILIVYOUA SITA, KUJERUHI TISA

WATU sita wamekufa na wengine tisa kujeruhiwa baada ya gari aina ya Nissan Caravan Hiace walilokuwa wakisafiria kuacha...

## Rais Samia apiga 'stop' usafirishaji korosho ghafi

UKURASA 3



Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo katika moja ya vyumba vya upasuaji baada ya kuzindua Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini, Mtwara jana. **PICHA: IKULU**



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Arusha, wakiangalia mabaki ya gari aina ya Nissan Caravan lenye namba za usajili T 135 DBC lililopata ajali katika eneo la Kisongo, jijini humo juzi jioni, baada ya kuacha njia na kugonga mti na kusababisha vifo vya watu sita na wengine tisa kujeruhiwa. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## D' Salaam yapoteza trilioni 1.4/- kila mwaka kisa foleni

UK. 2


**MICHEZO** SIMBA, YANGA LAZIMA KIELEWEKE UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kilio kila kona wananchi kukatika kwa umeme

**Na Waandishi Wetu**

NI kilio kila kona kutokana na kukatika kwa umeme. Hii ni baada ya wafanyabiashara na wananchi kulalamikia kukatika kwa umeme mara kwa mara huku wakisema hakuna taarifa yoyote kutoka mamlaka husika, hivyo kusababisha hasara na uharibifu wa vifaa na mitambo.

Nipashe ilipomtafuta jana, Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Nector Pendaeli, kuzungumzia suala hilo, alikiri kuwapo kwa tatizo baadhi ya mikoa.

"Kuna baadhi ya maeneo kwenye mikoa inafanyiwa matengenezo na maboresho ya miundombinu ya umeme ili kuimarisha hali ya upatikanaji umeme na taarifa za matengenezo hayo zitatolewa na ofisi za mikoa nchi nzima," alisema Pendaeli.

Baadhi ya wafanyabiashara na wakazi wa Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, wakizungumzia tatizo hilo, walisema limekuwa likijitokeza kila mara kwa wiki kadhaa sasa.

"Mfano juzi (Septemba 13, 2023) kuanzia asubuhi kulikuwa hakuna umeme hadi usiku wa saa 4:00. Mimi ni mfanyabiashara wa bucha la Samaki na samaki hawa nawahifadhi kwa kutumia umeme. Unapokuwa haupo siku nzima unaathiri biashara yangu na kunisababishia hasara," alisema mfanyabiashara Audax Munuo.

Baadhi ya wakazi wa Tanga walilalamikia hali kama hiyo kutokea mkoani humo wakisema imekuwa ikitokea katika maeneo mengi na wengine kupata madhara ya kunguliwa na vifaa.

Mfanyabiashara wa duka la vinywaji baridi, John Pesambili, alisema: "Hali hii sasa inatuchosha na imeonekana kama ni kawaida sana. Ilianza kidogokidogo na sasa imekuwa kawaida. Imefikia mahali tunaunguza hata vifaa vyetu vya ndani kwa sababu hatujui ni wakati gani unakatika au unarudi.

Mkazi wa Jiji la Arusha, Ayubu Andrew, alisema jijini humo tatizo hilo kwa sasa limedumu kwa takribani mwezi mmoja na hakuna sababu iliyotolewa kwao.

Alisema kwa hali ilivyo wanaona kama kuna mgao wa kimyakimya lakini mamlaka husika mpaka sasa haijatoa taarifa.

Mfanyabiashara Rahim Adam, ambaye anauza sharubati na matunda, alisema biashara yake imekuwa ikiathiriwa na tatizo hilo kwa kuwa hutegemea zaidi umeme.

Mkoani Morogoro, wananchi mkoani humo wamesema wameanza kuonja makali ya kukatika kwa umeme takribani wiki moja sasa.

Katika maeneo ya Kihonda Maghorofani, Mazimbu, Kingo, Kichangani, Kilakala na Mbuyuni, umeme umekuwa ukikatika kuanzia majira ya saa 2:00 asubuhi na kurejea saa 12:00 jioni na maeneo mengine umekuwa ukikatika saa 1:00 usiku na kurejea saa 6:00 usiku.

Mfanyabiashara wa samaki na kuku eneo la Kihonda, Amani Masige, aliomba mamlaka husika kutoa taarifa kuhusu sababu ya kukatika huko kwa umeme mara kwa mara ili wajipange.

Mmiliki wa duka la dawa, Kata ya Nyasubi, Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Paschal Njamba, alisema wanapata wakati mgumu kuhifadhi dawa ambazo zinahitaji ubaridi.

Naye mmiliki wa kiwanda cha kutengeneza samani za ndani, Zacharia James, alisema eneo lao la viwanda, maarufu kama Dodoma, shughuli zimesimama kwa ukosefu wa umeme huku Yulitha Elisonguo, mkazi wa Nyamagana, akisema: "Hatujui kama ni mgawo au la. Hali hii inakera sana. wanakata bila kutoa taarifa wakati mwingine tunaunguza vyombo vyetu."

Elizabeth Boniphace, mfanyabiashara wa wa barafu na maziwa ya mtindi alisema kukatika kwa umeme wilayani Maswa, kumeathiri kwa kiwango kikubwa na kumsababishia hasara.

Meneja wa TANESCO Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu, Mhandisi Issack Fimbo, akizungumza na Nipashe jana, aliwaomba radhi wateja kutokana na adha hiyo ambayo imekuwa mwendelezo kwa zaidi ya mwezi sasa, akibainisha kwamba sababu ni mgawo wa umeme kitaifa.

Pia alisema suala la kukosa kituo cha kupokelea na kupoza umeme wilayani humo nacho kinachangia kwa kiasi kikubwa athari za kukatika kwa umeme huo. Hata laini ya Ibadakuli mkoani Shinyanga nayo imeshazidiwa. Hii hali inatufanya kushindwa kuwatangazia wananchi ratiba ya mgawo wa umeme," alisema Mhandisi Fimbo.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Simiyu, Mhandisi Alistidia Clement, aliiambia Nipashe kuwa kukatika kwa umeme mara kwa mara katika mkoa huo kunatokana na kuongezeka kwa mtandao wa huduma ya umeme kwa zaidi ya kilomita 1,600 mwaka 2023.

Alisema mwaka jana mtandao wa umeme ulikuwa kilomita 1,800 na sasa umeongezeka baada ya mkoa huo kufanikisha kusambaza umeme katika mitaa na vijiji vyote zaidi ya 400 vya mkoa, hivyo matumizi kuongezeka na kusababisha uimara wa miundombinu kupungua.

**Imeandikwa na Anjela Mhando (K'njaro), Hamida Kamchalla (Tanga), Allan Isaack na Tumaini Mafie (Arusha) Ashton Balaigwa na Christina Haule (Moro), Shaaban Njia (Kahama), Neema Emmanuel (Mwanza), Alex Sayi (Maswa), Ndalike Sonda (Bariadi), Said Sindo (Geita) na Beatrice Shayo (Dar)**


**ARM SOLUTION AUCTION MART AND PROPERT MANAGEMENT CO LTD**

**MNADA WA HADHARA**

KWA IDHINI TULIYOPEWA NA MuCoBa Bank Plc.TUNAWATANGAZIA WANANCHI WOTE KUWA KUANZIA TAREHE 28-09-2023 NA KUENDELEA TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MALI ZA WADAIWA HAPO CHINI ILI KUFIDIA MADENI WANAYODAIWA.

| NO | JINA LA MDAIWA | TAWI ALILOKOPA | DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA/ MUDA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | FILBET YOVENARY KALINGA | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA UPENDO -MTAA WA BALALI (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 2. | ANJELO ANDREAS NYEMBEKE | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA BOMA – (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 3. | LUCAS LEVES MSINGWA | IRINGA | NYUMBA | KATA YA CHANGALAWE-MTAA WA BLOCK J (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 4. | REUBEN MWAKASALA | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA BOMA-MTAA WA IHONGOLE (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 5. | FABIAN GODFREY NYERINDE | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA BOMA-IHONGOLE (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 6. | EMMANUEL R WISSO | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA UPENDO -MTAA WA BALALI(MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA O3 ASUBUHI |
| 7. | VAILETH GEORGE HAULE | MAFINGA | NYUMBA | MAKWAWA -LUNGEMBA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 8. | GODWIN DITRICK MHESI | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA UPENDO -MTAA WA BALALI (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 9. | DANIEL DITRICK MHESI | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA KINANYAMBO - MTAA WA GANGILONGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 10. | GODFREY MHAGAMA | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA BOMA- MAFINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 11. | CHARLES MASHITA | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA BOMA- MTAA WA IHONGOLE | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 12. | FANTI MWELELA | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA CHANGALAWE | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 13. | JOCTAN NYALUKE | MAFINGA | NYUMA | KATA YA BOMA- MTAA WA IHONGOLE | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 14. | GASTON NTAMAKILILO | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA LUNGEMBA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 15. | AMOS SANGA | MAFINGA | NYUMBA | ILULA - IRINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 16. | MENERICE BEAUTUS BALAMA | MAFINGA | NYUMBA | KILOLO- IRINGA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 17. | ABDALLAH MSAFIRI NZINGO | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA CHANGALAWE-MTAA WA BLOCK J (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 18. | HAJI NYAKWILOLA | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA BOMA -MTAA WA MALINGUMU | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 19. | MUSA MAKWETA | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA CHANGALAWE | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 20. | METHEW NALOLE | MAFINGA | PAGARE LA NYUMBA | KATA YA CHANGALAWE | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 21. | MARIAM HAWARD NG'UMBI | MAFINGA | NYUMBA | KATA YA BOMA-IHONGOLE (MAFINGA) | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |
| 22. | ALEXANDER JOHN SEIYAI | MAFINGA | SHAMBA NA PAGARE | KATA YA BOMA | NA KUENDELEA KUANZA SAA 03 ASUBUHI |

**MASHARTI YA MNADA**

MSHINDI ATATAKIWA KULIPA ASILIMIA (25%) AU ZAIDI BAADA YA NYUNDO YA DALALI NA BAKI (75%) ITALIPWA NDANI YA SIKU KUMI NA NNE (14), TOFAUTI NA HAPO MSHINDI ATAPOTEZA HAKI ZAKE NA MNADA UTARUDIWA UPYA.

**MAWASILIANO: 0757 -107 715, 0784 -759 892**

217603702


# Dar yapoteza tril. 1.4/- kwa mwaka kisa foleni

**Na Halfani Chusi**

KAMISHNA wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP), David Kafulila, amesema jiji la Dar es Salaam linapoteza wastani Sh. trilioni 1.4 kwa mwaka kwa kutokana na msongamano wa magari barabarani.

Kafulila aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akiwakaribisha wawekezaji katika sekta mbalimbali ikiwamo ya uchukuzi.

"Wingi wa watu katika Jiji la Dar es Salaam unazidi eneo. Watu ni wengi kuliko eneo. Sehemu ya kutumia dakika 10 unatumia dakika 50 kufika," alisema.

Kuhusu mkakati wa serikali kupunguza foleni, alisema kwa sasa serikali inaangalia namna ya kualika wawekezaji katika reli ya Dar es Salaam ili kujenga barabara za kutoa watu katikati ya jiji na zile zinazoingia na kutoka na kwamba kukamilika kwa mpango huo kutaokoa upotevu wa fedha.

Aliwataka Watanzania kutofautisha kati ya mkataba wa ubinafsishaji na ubia huku akisema serikali inapoingia ubia, umiliki hauhami bali unabaki ndani ya serikali.

Kafulila aliutaja mpango wa serikali katika kuwavuta wawekezaji kwa sasa kuwa umeanzishwa utaratibu wa kila Alhamis na Ijumaa kusikiliza mawasilisho manne mpaka sita ya watu au kampuni zenye nia ya kuwekeza na atakayekidhi vigezo, wanaingia naye kwenye makubaliano.

Alisema kampuni binafsi zinapowekeza nchini zinaongeza mzunguko wa fedha za kigeni, ajira kwa vijana na kuchochea ukuaji wa uchumi kwenye eneo husika.

"Kuna kampuni ambazo tayari zimeonyesha nia ya kuwekeza katika reli ya Dar es Salaam. Tumewaambia wakalete maandiko yao ili tuyapitie tuone kama yako sawa au la. Kuna kampuni kubwa zimeomba, moja ya kutoka Uturuki na nne za China kwa hiyo zinaandaa proposal (dokezo). Kampuni itakayoshinda ndiyo itapewa," alisema.

Kafulila aliwataka wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuchangamkia fursa za uwekezaji nchini kabla serikali haijatangaza na kutolea mfano mradi wa reli wa Morogoro-Dodoma kwamba bado haujapata mwekezaji.

HABARI KITAIFA

# Samia apiga 'stop' usafirishaji korosho ghafi

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema miaka miwili ijayo korosho hazitasafirishwa zikiwa na magamba badala yake zitabanguliwa na kusafirishwa kutokana na mpango mkubwa wa ujenzi wa viwanda.

Aliyasema hayo jana akiwa katika ziara mkoani Mtwara na kusisitiza kuwa korosho hizo ni lazima zibanguliwe ndipo zisafirishwe. "Korosho zitabanguliwa ndipo zisafirishwe. Tuna mpango mkubwa wa kujenga viwanda. Tutabangua korosho na kuisafirisha ikiwa imebanguliwa. Hayo ndiyo malengo yetu. Suala la meli tutahamasisha sekta binafsi tuone namna watakavyoweza kufanya.

"Kilio cha wananchi ni suala la korosho na sasa korosho isafirishwe kutoka Bandari ya Mtwara. Mimi sielewi ni nini kinawazuia watu wa Mtwara kusafirisha korosho kwa sababu Bandari wameeleza wako tayari kusafirisha na hadi makasha yapo,"alisema.

Rais Samia alisema mwaka jana alijulishwa hakuna makasha na ilipofika mwaka huu tayari kuna makasha 112 na mengine yanapelekwa kuna huko.

"Niwaombe sana wana Mtwara hasa viongozi. Yale ambayo yalikuwa yanazuia korosho kusafirishwa kupitia bandarini kaeni mkubaliane. Najua kuna wafanyabiashara wenye malori yao ambayo yanabeba korosho kuleta mjini au Dar es Salaam na pia kuna wenye vituo vya mafuta. Korosho ikisafirishwa kwa meli hawatapata malori ya kujaza mafuta huku,"alisema.

Pia alisema kuna mambo tofauti ya uchakachuaji wa korosho yanayofanywa njiani wakati zikisafirishwa kwa gari, hivyo kuharibu sifa ya zao katika soko la dunia.

Rais alisema msimu wa korosho unaanza Septemba 20, mwaka huu, hivyo wanasubiri kuona ni kazi gani itakayofanywa kusafirisha bidhaa iyo kupitia Bandari hiyo.

Pia aliwaagiza mkuu wa mkoa huo na Jeshi la Polisi kuhakikisha anayesafisha korosho kwa gari awe na kibali cha mkuu wa mkoa, kwa kueleza sababu za kutumia usafiri huo na zinakoelekea ili kupata takwimu sahihi.

"Watajua korosho zimetoka hapa zimekwenda wapi? Mkuu wa mkoa najua upo mjini na una wakuu wa wilaya. Kama watashindwa kusimamia hiyo kazi niambie nikuletee watenda kazi kufanya kazi hiyo vizuri. Hakuna sababu ya kwa nini korosho zisisafirishwe kupitia Bandari," alisema.

Rais Samia alisema jambo la msingi ni kuhakikisha wanaipa thamani korosho ili wasiendelee kupata aibu ya kila mwaka ya kuonekana na uchafu.

**HOSPITALI YA KANDA**

Akizungumzia kuhusu uzinduzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini alioufanya jana, Rais Samia alisema amejionea mambo yanayofanyika kuwa ni ya aina yake na ina vifaa vya kisasa ambavyo vitasadia kuhudumia mikoa mitatu ya Ruvuma, Lindi na Mtwara.

"Ni hospitali maalumu yenye kuhudumia magonjwa makubwa, watu wakishindikana katika hiyo mikoa basi watakwenda hospitalini hapo, tayari serikali imeshatengeneza mambo mazuri katika kutoa huduma kwa wananchi," alisema

Alisema jambo lililomfurahisha ni huduma ya kusafisha figo kwa Kanda ya Mtwara na tayari vifaa vimefika, hivyo huduma itapatikana na masuala ya moyo na huduma nyingine za kitaifa zitatolewa katika hospitali hiyo.

Rais Samia alisema tayari kuna vifaa vya kufanya vipimo vya saratani, hivyo hakuna sababu kwa watu waliopo katika mikoa hiyo kuja kupatiwa matibabu kwa mkoa wa Dar es Salaam na kwamba kwa sasa watakwenda jengo la huduma za mama na mtoto.

"Nataka wajenge kiwanda cha kutengeneza yale maji wanayowawekea wagonjwa badala ya kwenda kuchukua huko wanakokwenda kuyafuata," alisema.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA
Tarehe: 15/09/2023

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumapili tarehe 17-09-2023** kampuni ya **HAINAN INTERNATIONAL LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM** kuelekea **MTWARA**, Gari hilo lenye namba za usajili: **T 175 DFN/T 168 DFN**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **18:00** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.80** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.00** |

3. Njia itakayotumika **DAR ES SALAAM hadi MTWARA kupitia KILWA ROAD.** Gari itasafiri muda wa mchana tu ***( kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka 12:00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakao jitokeza.***

217603802





Mkuu wa wilaya ya Nachingwea, mkoani Lindi, Mohamed Moyo, akikagua gwaride wakati wa kufunga rasmi mafunzo kwa mujibu wa sheria ya operesheni miaka 60 ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Kambi ya 843 KJ Nachingwea, hivi karibuni. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Dada wa kazi adai kuahidiwa mil. 50/-

**Na Grace Gurisha**

DADA wa kazi wa marehemu Aneth Msuya, Getruda Mfuru, juzi aliiambia mahakama kuwa aliyekuwa mke wa Erasto Msuya, maarufu kama Bilionea Msuya, Miriam Mrita, aliahidi kumpa Sh. milioni 50 endapo angeondoka nyumbani kwa bosi wake ili afanye kazi yake.

Mfuru (38) ambae ni shahidi wa 25 katika kesi ya mauaji namba 103 ya mwaka 2018 dhidi ya Mrita na mfanyabiashara Revocatus Muyela, alidai hayo mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akitoa ushahidi wake.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Paul Kimweri, Mfuru alidai kuwa ahadi hiyo alipewa na Mrita Mei 23, 2016 alipokwenda nyumbani kwa Aneth, baada ya kupigiwa simu na mama huyo kuwa waonane nje ya nyumba.

Mfuru alidai kuwa alipotoka nje alikwenda kwenye gari lililokuwa limesimama na alipofika aliegemea kioo cha gari ambacho kilishushwa na alipoangalia ndani alimwona Mrita akiwa amekaa kiti cha pembeni.

"Aliyekuwa amekaa siti ya dereva ni yule baba (Muyela) ambaye alikuwa anakuja mara kwa mara Kibada Kigamboni kwa dada yangu Aneth. Nilipotazama vizuri ndani ya gari niliona vijana wanne.

"Vijana hawa walikuwa wamevaa soksi nyeusi kichwani na walikuwa wamezitoboa macho na pua huku wakiwa wamevaa makoti meusi na mmoja wao alikuwa ameshika 'briefcase'," alidai.

Mfuru alidai kuwa kilichoendelea yule aliyekuwa ameshika 'briefcase', aliifungua na aliona noti za Sh 10,000 zikiwa zimefungwa na 'rababendi' na yule mama (Mrita) alimwambia kuwa hizo ni Sh. bilioni 50.

"Baada ya kuona fedha hizo, yule mama (Mrita) aliniambia "hizi fedha hivi karibuni zinakuwa zangu endapo nitaondoka pale nyumbani ili afanye kazi yake. Lakini hakunieleza kazi ambayo anakwenda kuifanya kwa Dada Aneth," alidai.

Alidai kuwa wakati Mrita anamwambia maneno hayo, yule aliyekuwa ameshika 'briefcase' alishika bastola na kumwekea kifuani hali iliyomfanya aogope sana na aingiwe na hofu na kwamba hayo yote wakati yanatokea alikuwa ameegemea kioo.

"Baada ya haya yote yule mama aliniambia kabla ya Mei 25, 2016 kufika niwe nimeondoka nyumbani kwa Dada Aneth kwa sababu kuna kazi anakuja kuifanya. Alinipa Sh 20,000 na kuhusu Sh. milioni 50 aliniambia atanipatia Arusha," alidai.

Pia alidai kuwa jambo lingine Mrita alilomwambia ni kuhakikisha simu aliyompa haionekani na mtu yeyote na ikiwezekana aitupe kabisa isionekane.

"Ilipofika Mei 25, 2016 majira ya saa 5:30 asubuhi, niliondoka nyumbani kwa dada na Kwenda Feri Kigamboni kwa lengo la kuonana na rafiki yangu Sabri Kombo. Wakati natoka nilifunga mlango wa nyumba na kuweka ufunguo chini ya zulia. Niliweka hapo kwa sababu mimi na dada Aneth ndipo tulikuwa tunaweka. Baada ya hapo nilifunga geti kubwa la fensi na kuondoka na funguo," alidai

Mfuru alidai alipanda daladala kutoka Kibada hadi Feri na alipofika alipanda pantoni Kwenda Magogoni kukutana na rafiki yangu Sabri Kombo na kwamba wakati yuko kwenye pantoni akakumbuka maneno ya yule mama kuhusu simu, akaitupa ndani ya maji.

"Nilipofika Magogoni nilikutana na Sabri, nilimwomba kwa siku hiyo nikalale kwake Chanika. Aliniambia dada yako Aneth hataleta shida? Nikamwambia hana shida, nikakumbuka kwamba ufunguo wa geti kubwa ninao, nikamuomba Sabri anisindikize niurudishe," alidai.

Alidai kuwa alikutana na mwanafunzi wa shule ya msingi akampa ufunguo huo aupeleke kwa jirani yao ambapo huwa wanachota maji. Alipoipeleka yeye aliondoka na pikipiki akiwa na Sabri hadi Chanika.

"Niliondoka nyumbani kwa sababu yule mama aliyenipa simu ya Nokia (Mrita) aliniambia akinikuta mle ndani ataniwajibisha na pia kutokana na vitisho nilivyopewa na kunyooshewa bastola .

Pia, alidai kuwa alipokuwa nyumbani kwa Sabri, Aneth alimtumia ujumbe mfupi kwenye simu kuwa: 'Getruda hebu rudi nyumbani uondoke kwa usalama', lakini hakumjibu chochote.

Alidai kuwa Mei 26,2016 majira ya saa nne asubuhi alipigiwa simu na ndugu yake Neema kutoka Mererani kuwa Dada Aneth ameuawa kinyama nyumbani kwake Kigamboni na kwa bibi Msuya kumejaa watu wengi sana.

Shahidi huyo alidai kuwa Mei 27, 2016 hakukamatwa na polisi alikuwapo nyumbani kwa Sabri na Julai 20,2016 akiwa nyumbani kwao, Masama, alipigiwa simu na Bibi Msuya, akimuulizia yuko wapi.

Alidai kuwa Julai 23,2016 alipigiwa simu na askari polisi nakumueleza kuwa yupo nyumbani kwao, Julai 24, 2106 alipanda gari na askari wawili wa kike na wa kiume

Shahidi huyo aliulizwa maswali ya dodoso na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, kama ifuatavyo;-

**Kibatala:** Mrita alikaa muda gani kwa wakwe zake hiyo mwaka 2015?

**Shahidi:** Alikaa muda mchache na kuondoka.

**Kibatala**: Uliona dalili zozote za ugomvi kati ya Mrita na wakwe zake?

**Shahidi:** Sikuona dalili zozote za ugomvi.

**Kibatala:** Moja ya magari ambayo Mrita alikuwa anakuja nayo mara kwa mara Kigamboni, ndiyo moja ya magari aliyokuja nayo Mererani?

**Shahidi:** Mimi sikuona gari ambalo alikuja nalo.

**Kibatala:** Ile nyumba yenye duka ilikuwa ina ukuta?

**Shahidi:** Ndiyo.

**Kibatala:** Unakumbuka nyumba ya Aneth ilikuwa na vyumba vingapi?

**Shahidi:** Sikumbuki.

Kesi hiyo iliahirishwa jana kwa ajili ya shahidi kuendelea kuulizwa maswali ya dodoso na mawakili wa utetezi.

## 'Mahakama mdau muhimu wa fidia'

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

MAHAKAMA imeelezwa kuwa ni chombo muhimu katika mchakato wa ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma, alisema hayo jana jijini hapa wakati akifungua kikao kazi cha kimkakati baina ya WCF na watendaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Kanda ya Ziwa na Wakurugenzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA), ili kuwajengea uelewa wa sheria ya fidia kwa wafanyakazi.

Alisema mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya serikali ya kuzitaka taasisi za umma kuongeza ufanisi na ubora wa utoaji huduma kwa wananchi. Kikao kama hiki kilifanyika Juni 9, mwaka huu, mjini Bagamoyo na kiliwakutanisha watendaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi Kanda ya Dar es Salaam na Pwani na wale wa CMA Kanda ya Dar es Salaam.

"Kwa hivyo mahakama na CMA ni wadau muhimu katika utekelezaji wa sheria ya fidia kwa wafanyakazi lakini pia tunajenga uelewa wa pamoja... kikao kazi hiki kitaleta manufaa makubwa ikiwamo kuimarisha uhusiano kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi na kuchangia kwenye kukuza uchumi wa nchi yetu," alisema.

Jaji Mfawidhi Mahakama Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi, Dk. Yose Mlyambina, aliipongeza WCF kwa kuwa tayari kushirikiana na mahakama na taasisi zinazohusu utatuzi wa migogoro ya kazi.

Alisema mafunzo hayo yatasaidia taasisi hizo kubadilishana uzoefu kwenye mambo ya sheria zinazohusu ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi wanaoumia au kuugua wakiwa kazini au kwa familia za wafanyakazi wanaofariki kutokana na ajali wakiwa kwenye maeneo yao ya kazi.

"Mheshimiwa Jaji Mkuu alifanya ugatuzi kwa kuelekeza majaji wote wa Mahakama Kuu ya Tanzania, naibu wasajili na mahakimu wakazi wafawidhi wote sehemu ambazo hazina masjala za Mahakama Kuu kushughulikia mashauri ya kazi, hivyo niliwaomba WCF watuandalie mafunzo mengine ya kikanda na nashukuru leo tuko hapa Mwanza," alisema.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa CMA, Thomas Malekela, alisema tume inashughulika na haki zilizovunjwa mahali pa kazi.

"Mfanyakazi anaweza akalalamika juu ya mshahara ambao kwa kweli si wenyewe. Anazungumzia mshahara pamoja na maslahi, mimi nikatoa uamuzi kuwa mshahara wako halisi ni huu, hivyo WCF itatumia uamuzi huo wa CMA ambayo ndiyo itatumika katika kutekeleza jukumu lake la kulipa fidia," alisema.

Pamoja na kujifunza sheria ya fidia kwa wafanyakazi, maeneo mengine ambayo majaji hao na wakurugenzi wa CMA wamejifunza ni taratibu za madai na wamepata fursa ya kuelezwa jinsi tathmini za madhara ambayo mfanyakazi ameyapata inavyofanyika.

# Ajali Hiace ilivyoua watu sita, kujeruhu tisa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WATU sita wamekufa na wengine tisa kujeruhiwa baada ya gari aina ya Nissan Caravan Hiace walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kuparamia mti katika eneo la Kisongo mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alisema gari hilo maarufu kama kipanya lenye namba za usajili T 135 DBC lilipata ajali wakati likitoka Wilaya ya Karatu mkoani Manyara kuelekea jijini Arusha.

Masejo alisema ajali hiyo ilitokea juzi saa 11:30 jioni baada ya dereva kupoteza mwelekeo na kushindwa kulimudu, kisha kwenda kuparamia mti.

"Katika ajali hiyo watu sita wamefariki dunia, kati yao wanawake ni wawili na wanaume ni wanne. Majeruhi wa ajali hii ni watu tisa wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufaa ya Mount Meru. Miili yote imehifadhiwa hospitalini hapo kwa ajili ya kusubiri ndugu kuitambua," alisema.

Shuhuda wa ajali hiyo, Denis Mollel alidai kuwa ilitokea wakati dereva wa kipanya hicho akijaribu kulipita lori lililokuwa mbele yake kwenye eneo hilo ambalo haliruhusiwi huku akiwa kwenye mwendokasi.

Alisema akiwa katika harakati hizo, alikutana na uso kwa uso na lori aina Benz na kukosa mwelekeo kisha kugonga mti.

Akizungumza baada ya kuwajulia hali majeruhi, Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, aliwataka madaktari kutoa huduma nzuri ili afya zao ziimarike haraka.

"Madereva wanaotumia vyombo vya usafiri wawe makini zaidi na kuhakikisha magari yanayobeba abiria yamefanyiwa ukaguzi wa kina ili kuepuka ajali zisizo za lazima zinazopelekea kupoteza nguvu kazi ya Taifa kutokana na watu kufa," alisema.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mount Meru, Frank Shega, alisema kati ya majeruhi hao waliowapokea, wawili hali zao siyo nzuri wamelazwa chumba cha wagonjwa wanaohitaji uangalizi maalumu (ICU).

Dk. Shega alisema majeruhi wengine wamepata majeraha mbalimbali, wakiwamo waliofanyiwa upasuaji kutokana na kuvunjika miguu na mikono.

Mmoja wa majeruhi hao, Joyce Laizer, alisema ajali hiyo ilitokea wakati dereva wao akijaribu kulipita lori hiyuo huku akiwa kwenye mwendokasi bila ya kuchukua tahadhari.

Joyce alisema ameumia kifuani kutokana na kubanwa na kiti wakati ajali hiyo ikitokea. "Tulikuwa tunatoka kwenye mahafali ya mtoto wa kaka yangu aliyekuwa amehitimu mafunzo ya miezi mitatu ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) Makuyuni," alisema.

# Wadau wa demokrasia wataka mgombea binafsi

**Na Sabato Kasika**

BAADHI ya wadau wa demokrasia wameeleza matamanio yao ya kutaka kuwapo kwa mgombea binafsi na kuweka usawa wa kijinsia kwenye uongozi.

Wadau hao walipaza sauti zao jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Demokrasia ulioratibiwa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) huku wakitaka suala la mgombea binafsi kufanyiwa kazi.

Katika mkutano huo, kulifanyika uzinduzi wa kitabu kiitwacho, Miaka 30 ya Demokrasia ya Vyama Vingi nchini Tanzania 1992 mpaka 2022. Tafakari ya Maendeleo, Changamoto na Fursa. Miongoni waliohudiria ni wanasiasa na asasi za kiraia.

Mkurugenzi Mtendaji Mstaafu wa LHRC, Dk. Hellen Kijo-Bisimba, alisema suala la mgombea binafsi halikwepeki na kwamba, ni muhimu kwa ustawi wa demokrasia nchini.

"Katika kitabu chenu kilichozinduliwa leo (jana) kikielezea kupanda na kushuka kwa vyama vya siasa, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Dk. Anna Henga, amegusia kesi ya mgombea binafsi ambayo hadi leo haijulikani ni nini kinakwamisha uwapo wa mgombea binafsi.

Alisema ndani ya vyama kuna changamoto nyingi zikiwamo ambazo zinakwamisha baadhi ya watu wenye nia ya kuongoza, kushindwa kufanya hivyo.

"Miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi tumeshuhudia namna ambavyo vyama vimekumbana na vikwazo ikiwamo suala la mgombea binafsi na hatuoni sababu ni kwa nini utaratibu huo usiwapo," alisema.

Katibu wa Baraza Kuu la Wanawake wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) (BAWACHA) Catherine Ruge, alisema wapo wanawake wanaotaka kuongoza, hawataki kupitia katika vyama vya siasa lakini wanakwama kutokana na mfumo wa sasa.

"Kuna haja ya kuwaacha Watanzania wawe huru kuchagua viongozi wao wanaotokana na vyama na wale wasiotokana na vyama," alisema Catherine.

Mwenyekiti wa Baraza la Vijana CHADEMA (BAVICHA), John Pambalu, alisema katika miaka 30 ya mfumo wa vyama vingi, nchi imeshindwa kuandika Katiba Mpya.

Katibu wa Shirika lisilo la kiserikali la Ulingo, Dk. Ave Maria Semakafu, alisema miaka 30 ya vyama vingi vya siasa nchini, hakuna uwiano katika uongozi, na wanawake waendelea kubaki katika nafasi za viti maalum.

"Ingawa katika kitabu kilichozinduliwa kinaelezea kuwapo kwa hatua za uwiano. Ukweli ni kwamba, bado kuna haja kuhakikisha kunakuwa na usawa wa kijinsia. Tunataka usawa siyo wanawake waendelee kuwa wengi nafasi ya Viti Maalum," alisema Dk. Ave Maria.

Mwenyekiti wa Idara Wanawake na Watoto kutoka Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Nasiria Ally, aliwataka wanasiasa kutowatumia wenye ulemavu kwa manufaa yao.

"Kila wakati wa uchaguzi, wanasiasa huwafuata watu wenye ulemavu na kuwapa ahadi hewa ili wawape kura.

Ninaomba muache kufanya hivyo," alisema Nasiria.

Mwanasiasa mkongwe, Stephen Wasira, alizitaka asasi za kiraia kujikita zaidi katika kutoa elimu ya uraia kwenye jamii ili kuiongezea uelewa.

"Mmetueleza kuwa kwa miaka 30 ya demokrasia mmeshuhudia pia, kuzuiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura, lakini ninadhani jukumu lenu ni kutoa elimu ya uraia, kusaidia jamii kutambua haki yao," alisema Wasira.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF) Bara, Magdalena Sakaya, alisema kwa miaka 30 hali ya demokrasia imekuwa ikiyumba kwa kutegemea na utawala wa nchi uliopo.

"Kwa mfano, miaka ya nyuma, upinzani ulikuwa na wabunge na madiwani na wenyeviti wa mitaa wengi, lakini sasa ni wa chama kimoja," alisema Magdalena.

Alisema kuna haja kwa mkutano huo kutoka na mazimio ambayo yatasaidia kuifanya demokrasia iweze kustawi kwa manufaa ya Watanzania.


## NOTISI/TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD, NGOMENI AUCTION MART, REAL MASTER LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,YONO AUCTION MART &CO.LTD , SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muunganowa Tanzania, chini ya Benki ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| MWANZA | MTONDI SIAGI KICHELE | NYUMBA YENYE HATI MILIKI | NYAMALANGO -MWANZA | 25/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MBEYA | ROGIMWA AGRO COMPANY LIMITED | KIWANJA CHENYE HATI NAMBA 083KYL/1204 | ITETE KYELA MBEYA | 26/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MAIN | KWANZA KILWA MINING & PRODUCTS LTD | NYUMBA YENYE HATI NA.94894,KIWANJA NA.460 KITALU '47' | KIJITONYAMA | 20/09/2023 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| TEGETA | SHEILA CLEVELAND NKATA | NYUMBA | MBEZI LUIS | 12/10/2023 SAA 4:30 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEGETA | ALOYCE JOHN KAZIMBAYA | NYUMBA | MADALE NYAKASANGWE | 30/09/2023 SAA 05:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | HALIMA JUMA HAJI | NYUMBA | VIKINDU | 20/09/2023 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | CHARAMBE -MBAGALA | 26/09/2023 SAA 6:00 MCHANA NA KUENDELEA (MARUDIO) |

217604302

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.**0715868000/ 0655715138/ 0765999000/ 0787129539/ 0719351040**
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la heri wawakilishi wetu katika mashindano ya CAF, kazi bado

**WAWAKILISHI** wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Yanga leo jioni watakuwa na kibarua cha kutafuta ushindi kwenye michezo yao ya ugenini ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Endapo klabu hizo zitafanikiwa kupata ushindi wa jumla kwenye michezo yote zitafanikiwa kutinga hatua ya makundi ya mashindano hayo makubwa kwenye ngazi ya vilabu Afrika.

Kila timu zinazowakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa ya CAF wakiwemo Singida Big Stars wanaoshiriki michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, wameweka malengo ambayo wanapambana kuyafikia.

Simba na Yanga zimejiwekea malengo angalau kucheza hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Tunataka kuzikumbusha klabu zetu hizi, haijalishi ni matokeo gani watayapata kwenye michezo yao ya leo, wanapaswa kufahamu kazi bado haijaisha, zipo dakika nyingine 90.

Wapinzani wao, Power Dynamos ya Zambia itakayocheza na Simba, Ndola nchini Zambia na Al Merrikh ya Sudan itakayoumana na Yanga jijini Kigali, Rwanda, si timu za kuzibeza ni lazima tahadhari zichukuliwe kwa mabenchi ya ufundi ya timu zote.

Kikubwa kinachotakiwa kwa wachezaji wa timu hizi ni kutochukulia kuwa mchezo ndo umeisha, bado kuna kazi mbele ya dakika nyingine 90 za kujithibitisha uhakika wa kusonga mbele au kuondolewa.

Tunaamini matokeo ya michezo hii ya leo bado haijatoa picha kamili ya nani anaingia hatua ya makundi ya michuano hii mikubwa.

Kikubwa ni kujipanga zaidi na kuweka mikakati mizur i kuelekea kwenye mechi za marudiano ili malengo yatimie ya kuweza kutinga hatua ya makundi.

Wakati wachezaji wa timu hizi wakiingia uwanjani leo jioni, wakumbuke ahadi ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Samia Suluhu Hassan ya kuendelea kutoa zawadi ya fedha katika kila goli litakalofungwa.

Hili kuzipata fedha hizi za Rais Samia na zile watakazoahidiwa na viongozi wa klabu zao ni lazima jasho liwatoke uwanjani kwa kuzipigania timu zao katika michuano hii muhimu.

Simba wamekuwa na uzoefu mkubwa kwenye mashindano haya, ni kwa miaka minne mfululizo wamekuwa wakifuzu hatua ya makundi, lakini bado hilo haliwapi uhakika wa kirahisi wa kurudia kile walichozoea kukifanya.


Kadhalika kwa Yanga, wana muda mrefu tangu kufuzu hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, nao hicho hakiwezi kuwa kigezo cha wao kushindwa mwaka huu kufikia hatua hiyo, vyote vinawezekana kwa wachezaji wake kujituma uwanjani.

Tunaamini mwaka huu historia itawekwa kwa timu zote mbili za Tanzania kutinga hatua ya makundi ya michuano hii ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kama timu zetu hizi zitafuzu hii itakuwa rekodi nyingine nzuri kwa soka letu na hasa katika kuitangaza ligi yetu, na soka la Tanzania kwa ujumla wake.

Tunazitakia kila la heri klabu zetu zote zinazoshiriki michuano ya CAF kuanzia Simba na Yanga zinazoshiriki Ligi ya Mabingwa Afrika na Singida Fountain Gate FC ambao kesho watacheza na Future FC kutoka Misri kwenye kombe la Shirikisho Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kutochaguliwa kuchezesha Afcon kuwaamshe waamuzi wetu nchini

**WIKI** hii Shirikisho la Soka Afrika (CAF) lilitoa orodha ya waamuzi 65 watakaochezesha Fainali za Mataifa ya Afrika Januari mwakani nchini Ivory Coast.

Waamuzi 32 ni wa kati na 33 wa pembeni, lakini hakuna hata mwamuzi mmoja kutoka Tanzania.

Inafikirisha na kusikitisha kuona Ligi ya Tanzania ambayo inatajwa kuwa ni ya tano kwa ubora Afrika, lakini haina hata mshika kibendera mmoja.

Cha ajabu ni kwamba kuna ligi za nchi ambazo hata mashabiki wa Tanzania wanaziona ni ndogo lakini zimetoa waamuzi.

Mfano kuna mwamuzi kutoka Somalia, Burundi, Rwanda Comoro, Djibouti, achilia mbali wengine kutoka nchi kama Mauritius Sao Tome & Principe, Madagascar na kadhalika.

Kama ingekuwa kuna mchezaji ametoka nchini humo kuja Tanzania kucheza soka, mashabiki wangekuwa na wasiwasi naye kwa sababu si nchi ambazo soka lake limepiga hatua kubwa kama kulinganisha na Tanzania, lakini zimetoa waamuzi.

Kwa jinsi soka la Tanzania linavyoheshimika nje ya nchi kwa sasa halafu hakuna mwamuzi hata mmoja huwezi kupepesa maneno, ni aibu.

Hili ni doa kubwa kwenye soka la nchi yetu kwa sababu hata watesi wetu wanaweza kuanza kuwatilia shaka hata mabingwa na washindi wanaopatikana kama wanapatikana kihalali.

Ligi bora ambayo haina waamuzi wazuri ni sawa tu na mtu kuvaa suti halafu chini ana ndala au kandambili.

Nilitegemea ubora wa ligi yetu ungeendana na ubora wa waamuzi, lakini inavyoonekana kuwa nchi hii ina wachezaji bora wanaochezeshwa na marefa wasio bora.

Kuanzia mabosi wa waamuzi na mpaka marefa wenyewe sijui wanajisikiaje?

Kwa hili haiwezekani kabisa kujisikia vizuri, kwani tayari wamewapa fimbo mashabiki ya kuwapigia kila wanapochezesha mechi mbalimbali.

Tatizo liko wapi? Wapo wanaodai kuwa tatizo kubwa la waamuzi wa Tanzania ni lugha, kwani wengi hawajui kifaransa na wanaongea kingereza cha kubahatisha.

Inasemekana waamuzi wengi wanaochaguliwa na CAF ni wale wanaojua Kifaransa na Kiingereza halafu kuna waamuzi wanaojua kuongea lugha zote mbili.

Hata hivyo ninavyojua mimi mwamuzi kwanza anachaguliwa kwa kuweza kuchezesha soka vizuri, kutafsiri vyema sheria na utimamu wa mwili, vingine vinafuata baadae.

Wengine wanadai CAF wanapenda zaidi waamuzi warefu, huku Tanzania ikiwa na waamuzi wengi wafupi.

Inawezekana ikawa kweli, lakini kwa kiasi kikubwa waamuzi wa Tanzania wanaangushwa kwa kutoweza kutafsiri sheria, hasa wanapokwenda kuchezesha mechi za Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la Shirikisho pamoja na Ligi Kuu Tanzania.

Siku hizi Ligi Kuu Tanzania Bara inaonekana zaidi kuliko ligi nyingine yoyote katika ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

Hawajui kuwa wanaangalia, hivyo wanapofanya madudu yanaonekana vizuri tu.

Imefika wakati sasa waamuzi wa Tanzania kubadilika. Waache tabia ya kuzipendelea timu, uoga, rushwa, kutojiamini na kuwa na mamlaka wanapochezesha.

Mechi inabidi ichezeshwe na ijiamue yenyewe na si kuonekana kubeba timu.

Waamuzi wakichezesha kama mahakimu, kuwa na haki kwa pande zote mbili kwa timu kubwa na ndogo, ndipo wanapoweza kuanza kuangaliwa na CAF.

Hili sasa liwe somo kwa waamuzi wetu.

Watataka kuishia kuchezesha ligi kuu tu au kwenda mbali zaidi?

# Waliomaliza vifungo wafunzwa ujasiriamali

**Na Beatrice Philemon**

WANAWAKE 33 waliomaliza vifungo katika magereza ya Ukonga na Segerea wamepata elimu ya kuwasaidia katika nyanja mbalimbali za kuinua maisha yao.

Maeneo hayo ni ujasiriamali, usimamizi wa fedha, haki za wanawake katika jamii, jinsi ya kupata mikopo yenye riba nafuu ili kujitegemea kiuchumi, kijamii na wasirudie tena kufanya makosa ya kijinai.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika lisilo la Kiserikali linaloitwa 'Tanzania Prisoners Hope Foundation (TPHP), Lucas Mwimo, alisema hayo juzi wakati wa semina ya siku moja kwa wanawake waliomaliza vifungo kutoka gereza la Segerea.

Mafunzo hayo yalitolewa na wataalam kutoka kampuni mbalimbali kwa ufadhili wa shirika lisilo la kiserikali la 'Women Fund Tanzania Trust (WFTT) na yalihudhuriwa na maofisa ustawi wa jamii, kamishina msaidizi wa magereza, mkuu wa gereza la wanawake Segerea na wawakilishi kutoka WFTT.

"Tumeamua kutoa mafunzo haya ili nao washiriki kikamilifu kuchangia gurudumu la maendeleo ya taifa, kupunguza kuwanyanyapaa kwa sababu hawa bado ni wanadamu wanaostahili kupata huduma zote za kijamii na pia wasijione wapweke na hatimaye wakarudia tena makosa ya kijinai," alisema. Pia aliwaomba wanawake waliomaliza vifungo na wale waliotoka mahabusu kuunda umoja wao ili kuwawezesha wadau na serikali kuwasaidia kiurahisi na sauti zao kusikika kwa urahisi.

"Mnaweza kuanza na kundi hili dogo mkawa na viongozi wenu ili kusaidiwa kiurahisi mara wadau wanapojitokeza kutoa misaada. Sisi TPHF tutaendelea kuomba misaada kwa wafadhili wa ndani na nje ya nchi na itakapopatikana mtakuwa watu wa kwanza kukumbukwa," alisema.

Alishukuru shirika la WFTT kwa kufungua mlango wa ufadhili ambao umesaidia wanawake waliomaliza vifungo katika gereza la Segera kupata elimu ambayo itawasaidia kuanzisha biashara na kujitegemea kiuchumi.

Alisema shirika la TPHP litaendelea kutoa elimu, ushauri na huduma mbalimbali kwa wanawake na wanaume wanaotoka magerezani kadri watakavyokuwa wanapata misaada kwa wadau mbalimbali.

"Tangu tumesajiliwa hadi sasa tumeweza kutoa misaada mbalimbali kwa wafungwa waliotoka Segerea na Ukonga zikiwamo taulo za kike 288, katoni tano za sabuni za kuogea na kufulia, televisheni moja, elimu ya ushauri nasaha kwa wafungwa 1,800 na magodoro 50 ya kulalia wafungwa," alisema. Misaada mingine ni kumpatia kadi ya bima ya afya ya NHIF mfungwa mmoja wametoa Sh. 500,000 kwa mjasiriamali mmoja, ili aweze kununua mizinga kwa ajili ya ufugaji nyuki na kuuza asali na vifaa vingine.

Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo, alishukuru WFTT na TPHP kwa kuwapatia mafunzo ambayo yatawasaidia kuwa watu wengine na kutofanya tena makosa ya kijinai.

Aidha, aliwaasa kuacha kujinyanyapaa na kuanza maisha mapya katika jamii zao na wilaya ipo tayari kuwasaidia kupata mitaji.

"Mnaweza kujiunga katika kikundi na kuomba mikopo, tunao wataalam ambao watawasaida jinsi ya kuandika maombi ya mikopo, mkiwa wa moja ya maofisa mikopo wetu watawapatia mikopo na serikali itaweza kuwasaidia," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wanawake wenzake, Veronica Ndunguru alisema wanaomba serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali kama TPHF waone namna ya kuwasaidia kupunguza au kuondoa kabisa hasa changamoto ya ukosefu wa mitaji, ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo. Pia alisema jamii ielimishwe kuwapokea vizuri wanapotoka magerezani na wasihukumiwe kutokana na makosa waliyofanya siku za nyuma.



Shekhe Amri Haruna (kulia), akifafanua jambo kwa wananchi waliojitokeza kupata huduma mbalimbali za afya bure kwenye kambi ya siku tatu iliyodhaminiwa na Taasisi ya Khoja Ithna-Asher Jamaat, katika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Tanzania na Msumbiji zakubaliana kufanyia kazi matishio ya kiusalama

**Na Romana Mallya**

TANZANIA na Msumbiji zimekubaliana kutekeleza mambo mbalimbali katika maeneo ya ulinzi na usalama ikiwamo kufanyia kazi matishio ya ugaidi na kuimarisha mipaka.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Tax, aliyasema hayo juzi wakati akifunga kikao cha tano cha kamati ya pamoja ya ushirikiano katika sekta ya ulinzi na usalama baina ya nchi hizo kilichofanyika jijini Dar es Salaam kwa siku nne.

Alisema jambo kubwa walilokubaliana ni kuendeleza ushirikiano wao katika kupambana na masuala ya kiulinzi na usalama ambayo matishio yake hayatambui mipaka.

"Yapo matishio ambayo tunayafanyia kazi wenyewe ndani ya nchi, lakini yapo matishio ambayo yanavuka mipaka, lazima tufanye kazi kwa pamoja. Kama mnavyofahamu ugaidi ni moja ya matishio ambayo hayatambui mipaka.

"Huu ni mwendelezo wa ushirikiano wetu. Kama mnavyofahamu Tanzania na Msumbiji tumekuwa ndugu na marafiki tangu wakati wa kupigania ukombozi wa nchi na wao wanalitambua hilo na wametoa shukrani za dhati kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa ushirikiano uliowezesha kupambana na tishio la ugaidi," alisema.

Waziri Tax alisema Tanzania inashirikiana na Msumbiji kama nchi na pia kama Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na kusisitiza kwamba hali inaendelea kuimarika.

Alisema licha ya hali kuendelea kuimarika na kutulia lazima waweke mikakati ya pamoja na hivyo kupitia mkutano huo, wamekubaliana mambo mbalimbali ya kutekeleza katika maeneo ya ulinzi na usalama.

Alisema mikutano ya aina hiyo imekuwa ikifanyika kila mwaka na mwakani utafanyika nchini Msumbiji huku wakiendelea kutekeleza yale waliyokubaliana.

"Mnafahamu Tanzania na Msumbiji tuna mpaka wenye ukubwa wa takribani kilometa 800 ni kazi kubwa kuhakikisha tunaimarisha ulinzi," alisema.

Waziri Tax alisema kwa ujumla hali ya kiusalama nchini ni shwari lakini kutokana na matishio yamekuwa yakibadilika, lazima wakae macho.

Dk. Tax alitoa wito kwa wananchi kuhakikisha wanadumisha usalama na amani ya nchi kwa kufanya matendo sahihi na wanapoona viashiria watoe taarifa.

Pia aliwataka kujiepusha na vitendo vyovyote ambavyo vinaweza kuathiri amani na usalama wa nchi husika.

Waziri wa Mambo ya Ndani wa Msumbiji, Pascoal Ronda, aliahidi nchi yake itayasimamia vyema mambo ambayo wamekubaliana katika kikao, ili kuimarisha ushirikiano wa ulinzi na usalama.

Alisema mikutano hiyo ni muhimu kwa kuwa inasaidia kujadili na kubadilishana utaalamu wa namna ya kuimarisha uhusiano na kusaidia kupambana na majanga na matishio mbalimbali.

# Kikwete awanyooshea kidole maofisa utumishi

**Na Lusungu Helela,** BUNDA

Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, amewaagiza maofisa utumishi wa halmashauri zote nchini kuacha tabia ya kukaa ofisini na kufanya kazi kwa mazoea.

Badala yake, amewataka kutembelea ofisi za watumishi zilizoko katika kata na vijiji ili kutatua changamoto za watumishi walioko katika maeneo hayo.

Kikwete alisema hayo juzi wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, ikiwa ni siku yake ya tatu ya ziara anayoendelea kufanya mkoani Mara. Aliwataka maofisa utumishi hao kuleta matumaini kwa watumishi wenzao

Aidha, Kikwete alipiga marufuku tabia ya baadhi ya maafisa utumishi kutoa vibali vya kusafiri kwa watumishi kwenda Dodoma katika Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kufuatilia masuala yao binafsi ya kiutumishi ilhali kazi hiyo inawahusu wao.

Amesema watumishi hao hufika Dodoma kwa ajili ya kufuatilia kupandishwa madaraja, kubadilishiwa miundo na kada, kudai malimbikizo ya mshahara hatua ambayo inawanyima fursa wananchi kuhudumiwa na watumishi hao waliolazimika kusafiri.

"Acheni ile tabia ya kuonekana miungu watu. Tatueni matatizo ya watumishi," alisisitiza. Naibu Waziri Kikwete alisema maofisa utumishi katika halmashauri hizo ni lazima watambue wateja wao namba moja ni watumishi wenzao, hivyo ni lazima wawape kipaumbele katika kutatua kero zinazowakabili ili kupata matokeo makubwa.

"Katika ziara zenu mtakazojipangia za kutembelea vituo vya kazi hakikisheni mnatatua changamoto za watumishi wenu huku mkitumia nafasi hizo kuwapatia taarifa za fursa mbalimbali za kiuchumi na za kujiendeleza kielimu zinazopatikana kwa sasa," alisisitiza.

Alisema haipendezi kuona hata masuala madogo tu ya kiutumishi yanayowakabili watumishi wao yanasubiri hadi siku waziri au naibu waziri atoke Dodoma ndipo aende kuyatatua.

Kikwete aliwaeleza maofisa utumishi hao kuwa ni lazima wahakikishe utendaji kazi wao unakuwa wa kimkakati na si kufanya kazi kwa mazoea

Aliwakumbusha kuwa moja ya majukumu ya msingi kwa maafisa utumishi ni kuhakikisha watumishi wanaowaongoza wanatatuliwa kero zinazowakabili hata ikibidi kufika Dodoma wasisite kwenda.

"Maofisa utumishi hakikisheni mnajipangia ratiba ya kutembelea vituo vyenu, zungumzeni na kusikiliza kero za watumishi. Sitegemei nikija tena nisikie changamoto ndogondogo kutoka kwa watumishi wenu," alisisitiza.

# AICC kujenga vituo vinne vya mikutano

**Na Restuta James**

KITUO cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC), kinatarajia kujenga vituo vinne vya mikutano vyenye hadhi ya kimataifa katika miji mikubwa minne ili kuvutia zaidi utalii wa mikutano.

Wakati ikidhamiria kufanya hivyo, AICC inadai Sh. bilioni 7.4 kutoka kwa wateja zikiwamo Sh. bilioni 4.7 kutoka taasisi za serikali ambazo zimepewa huduma bila kulipia.

Mkurugenzi Mtendaji wa AICC, Balozi Ephraim Mafuru, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipokuwa akizungumza na waharir na waandishi wa habari ikiwa ni mwendelezo wa Msajili wa Hazina, kutambulisha kazi zinazofanywa na mashirika ya umma kwa jamii.

Alisema malengo ya muda mfupi na wa kati wa AICC inayomiliki pia Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Julius Nyerere (JINCC), ni kujenga kituo cha Mlima Kilimanjaro jijini Arusha (MK-ICC) kitakachokuwa na uwezo wa kuingiza watu 3,000 kwa wakati mmoja.

Tofauti na vituo vingine, alisema MK-ICC itakuwa na nyumba za marais, hoteli za nyota tano, sehemu ya maduka (shopping malls) na sehemu ya michezo.

"Tunakusudia kujenga vituo Dodoma na Zanzibar na pia kupanua JNICC. Lengo letu ni kuvutia utalii wa mikutano na tutafsiri kwa vitendo ndoto ya waasisi wetu ya kuileta dunia Tanzania ili kuiingizia nchi yetu fedha za kigeni," alisema.

Alisema ujenzi utafanywa na serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na kwamba kwa sasa kituo hicho kinafanya kampeni kubwa ya kuunganisha wadau wote ili mgeni apate huduma bora kuanzia kwenye migahawa hadi ndani ya mkutano.

Mafuru alisema takwimu za mtandao wa mikutano ya kimataifa (ICCA) zinaonyesha kwamba Tanzania imeendelea kufanya vizuri kwenye eneo la utalii wa mikutano ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika. Kati ya mikutano 180 ya kimataifa iliyofanyika Afrika mwaka jana, 18 ilifanyika Tanzania.

"Tumepata maombi mengi kutoka kwa nchi mbalimbali kuja Tanzania kwa mara ya kwanza. Miaka minne iliyopita tulikuwa nafasi ya 13 na tulikuwa na asilimia tano ya umiliki wa soko.

Sasa tumepanda hadi nafasi ya tano na tunamiliki asilimia 10 ya soko," alisema Mafuru.

Alisema wameweka lengo la kupokea mikutano 30 kwa mwaka na kuhakikisha kila mgeni anayetoka nje anatumia dola za Marekani 400 lengo likiwa kuongeza mzunguko wa fedha kwenye uchumi.

Kuhusu mapato, alisema yameongezeka hadi Sh. bilioni 1.1 mwaka jana kutoka hasara ya Sh. milioni 500 miaka michache iliyopita. Alisema mwaka jana kituo hicho kililipa kodi ya Sh. bilioni 2.250 serikalini.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa inayowakabili ni ulipaji hafifu wa taasisi za umma ambazo zinadaiwa asilimia 65 ya madeni ya kituo hicho.

"Kati ya wadaiwa hao, 20 taasisi binafsi, 17 ni taasisi za serikali. Ninawaomba wakuu wa taasisi kama mimi tulipe madeni," alisema Mafuru.

**MIPANGO**

Alisema ili kuongeza uwajibikaji wa watumishi, wanakusudia kusaini mkataba wa utendaji ambao utapitiwa kila baada ya miezi mitatu kutathmini kama kila mtumishi amefikia malengo ya kituo.

Mipango mingine kwa mujibu wa mafuru ni kuainisha vipaumbele na kuboresha nyumba walizonazo ili ziendane na soko, pia kupanua hospitali ya AICC.

Akizungumzia changamoto, Mafuru alisema AICC inakabiliwa na uchakavu wa miundombinu pamoja na taasisi nyingi za serikali kutolipa madeni kwa wakati.

"Tanzania ina kila kitu kinachoweza kuvutia na kushindana Afrika na duniani katika utalii wa mikutano kama tutawekeza vizuri kwenye miundombinu. Tuna hifadhi nyingi za Wanyama na vivutio vingine vinavyoweza kuwaburudisha wageni wanaohudhuria mikutano hii ya kimataifa," alisema.

Pia alisema wanafanya maandalizi ya mkutano mkubwa wa wafuga nyuki duniani ambao umepangwa kufanyika nchini mwaka 2027.




Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Tandi Lwoga (kulia), akibadilishana mkataba wa makubaliano ya ushirikiano na Meneja wa taasisi ya JR Institute of Information Technology, Isack Marandu baada ya kutiliana saini kwenye ofisi za CBE, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# CBE kutoa mafunzo ya akili bandia

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimeingia makubaliano na Taasisi ya Teknolojia ya Habari ya JR ambao itakiwezesha chuo hicho kutoa mafunzo ya akili bandia na usalama wa mitandao.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana kwenye chuo cha CBE baina ya Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Tandi Lwoga na Meneja wa JR Institute, Isack Marandu.

Akizungumza kwenye tukio hilo, Prof. Lwoga alisema ushirikiano huo utakuwa na manufaa makubwa kwa chuo hicho kwa kuwa Taasisi ya JR ambayo inafadhiliwa na taasisi ya Punjani Charitable Trust, imebobea kwa kiwango kikubwa kwenye eneo la teknolojia.

"Wamechukua walimu wetu 12 kwenye idara ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), ambao watawapa mafunzo yatajayotusaidia na sisi kuanza kufundisha masomo hayo kwenye mwaka wa masomo kuanzia mwakani," alisema.

Prof. Lwoga alisema walimu wa chuo hicho wanasoma masomo hayo kwa njia ya mtandao na wamekuwa wakisoma kozi tofauti tofauti ikiwemo ya akili bandia ambayo imekuwa hitaji kubwa kwenye sehemu mbalimbali duniani.

"Walimu wetu wanafanya stashahada ya juu ya intelijensia ya jamii, watatu wamekwenda kusoma stashahada ya juu ya usalama mitandao, wawili wanasoma stashahada ya juu ya uchambuzi wa taarifa na sayansi na mmoja anafanya stashahada ya juu ya intelijensia ya bishara," alisema.

Pia alisema walimu hao wa CBE watasoma kwa njia ya mtandao kwa muda wa miezi 12 na wakimaliza watakuja kuanzisha program hizo walizosomea kwajili ya kuanza kuwafundisha wanafunzi hao.

Alisema baada ya mafunzo hayo anatarajia CBE itaanza kutoa mafunzo yanayoendana sana na sayansi na teknolojia kwani dunia ya sasa inaendeshwa na teknolojia mbalimbali za kisasa ikiwemo ile ya akili bandia.

"Tunashukuru sana kwa ajili ya huu ushirikiano ambao utajengea walimu wetu uwezo kwaajili ya kuanza kutoa mafunzo mafupi mafupi, kufanya tafiti mbalimbali na kutoa ushauri wa kitaalamu na sisi wakimaliza tutaanza kutoa mafunzo kama hayo hayo," alisema Profesa Lwoga

Mkuu wa Idara ya Hesabu na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) wa CBE, Dk. Ahmed Kijazi, aliushukuru uongozi wa chuo kwa juhudi za kuona umuhimu wa idara hiyo kwenda mbele katika teknolojia hiyo ya kisasa kama akili bandia na usalama mitandaoni.

Alisema wataalamu wa fani hizo ni wachache na kwamba anaminani uhusiano wa CBE na JR kutaboresha ufundishaji na kupata wahitimu wengi wa fani hiyo maeneo mengi nchini.

"Si kwamba hawa walimu wakihitimu watakuwa na manufaa hapa CBE tu, watakuwa na msaada nchini kwa ujumla kwa sababu wataalamu ni wachache sana kwa hiyo watafundisha watu wengi na hatimaye tutapata wataalamu wengi wenye ujuzi wa aina hii," alisema

Naye Meneja wa JR Institute, Isack Marandu, alisema walimu wa CBE wanaendelea kupata mafunzo kwenye chuo hicho na kwamba wanatengeneza walimu ambao watakuwa msaada kwenye teknolojia ya kisasa kama ya akili bandia na usalama mitandao.

Alisema taasisi yao ina wataalamu wa kutosha waliobobea kwenye mafunzo ya akili bandia na usalama wa mitandaoni ambao wamekuwa wakitoa mafunzo hayo kwa njia ya mtandao.

Chuo cha CBE kina matawi katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya.

# Jela maisha kwa kubaka na kulawiti mtoto wa miaka 15

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MKAZI wa Kata ya Mwinyi katika Manispaa ya Tabora, Abuu Abdallah Salehe (28), amehukumiwa maisha jela baada ya kutiwa hatiani kwa makosa ya kumbaka na kumlawiti binti mwenye umri wa miaka 15.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya mkoani hapa, Demetrio Nyakunga, aliyeeleza kuwa mshitakiwa alifanya makosa hayo kwa pamoja Julai 3, 2023.

Alieleza kuwa mshtakiwa huyo, alitekeleza ukatili huo katika eneo la Kata ya Chemchem Mwafrika mkoani hapa majira ya usiku.

Alieleza kuwa kosa hilo ni kinyume cha sheria chini ya kifungu kidogo Namba 130 (I) na (ii) b kikisomwa kwa pamoja na kifungu kidogo namba 131 cha kwanza cha makosa ya jinai, sura 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Hakimu huyo alibainisha kuwa, hukumu hiyo ni kwa mujibu wa makosa ya ulawiti na ubakaji chini ya kifungu cha 154, kifungu kidogo cha kwanza (a) na cha pili.



## Mavunde ahimiza ukusanyaji maduhuli ya Serikali

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Anthony Mavunde, amewahimiza watumishi wa wizara hiyo kushirikiana ili kuongeza ufanisi na kufikia malengo waliyopangiwa ya kukukusanya maduhuli ya Serikali ya kiasi cha Sh. Trilioni moja kwa mwaka wa fedha wa 2023/24.

Mavunde, alisema hayo juzi jijini hapa, wakati akizungumza katika kikao cha watumishi wa wizara hiyo.

Alisema wizara hiyo ina vitu vikubwa vya kufanya ambavyo ni mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa na kukusanya maduhuli hayo kwa mwaka huo wa fedha.

"Ili kufikia malengo haya mawili tunapaswa kuimarisha ushirikiano wetu kama wizara pamoja na taasisi zote tano zilizopo chini ya wizara, hii itatusaidia kuwa na umoja na upendo baina yetu, ndani na nje ya ofisi. Niwaeleze tabia yangu binafsi, sipendi majungu kwa sababu mimi ni mhanga wa majungu, sitavumilia tabia ya kuharibiana kazi, tushirikiane kuimarisha sekta hii. " alisisitiza.

Alisema kupitia kaulimbiu ya Maono 2030, Madini ni Maisha na Utajiri, sekta hiyo inaenda kupiga hatua kubwa na kuheshimisha nchi kupitia rasilimali madini.

Pia, alisema Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) itaongezewa uwezo ili kupitia utafiti wa kina isaidie kufikia maono na malengo hayo.

"Mbali na sekta ya madini, taarifa hizi zitasaidia upatikanaji wa maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kilimo cha umwagiliaji, malighafi za viwanda, yaani tunaenda kufunganisha Sekta ya Madini na sekta nyingine, tutafikia malengo kwa kuwa na taarifa sahihi za kisayansi na sio kubahatisha, " alisema Mavunde.

Aliongeza kuwa wizara hiyo imepanga kusimamia Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) ili ifikie hatua ya kuwa miongoni mwa shirika kubwa barani Afrika katika shughuli za mnyororo wa sekta ya madini.

Naibu waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa alisema ili kufikia malengo ya maono, hakuna budi kuweka mipango na kutengeneza njia ya kuyafikia.

"Ni matumaini yangu kuwa maono mazuri aliyokuja nayo Mheshimiwa Waziri tutayawekea mpangokazi ikiwezekana hata tuwe na majumuisho ya kila mwezi, ili isionekane kuwa ni maono yaliyobakia kwenye makaratasi, lazima kila mtu kwa nafasi yake afanye kazi kwa ufanisi wa juu ili kufikia malengo tuliyojiwekea kufikia mwaka 2030," alisema Dk. Kiruswa.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Kheri Mahimbali alisema watahakikisha wanasimamia ukusanyaji wa maduhuli kama ilivyopangiwa na Serikali Sh. Trilioni moja kwa mwaka 2023/24.

Mahimbali alisema watumishi watafanyia kazi kwa maelekezo na miongozo waliyopewa na wizarta hiyo ili kufikia malengo.

# CCWT yazinyooshea kidole kamati za ulinzi, usalama

**Na Paul Mabeja,** CHEMBA

CHAMA cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kimesema kamati za ulinzi na usalama za wilaya nchini zimeshindwa kutimiza wajibu wa kusababisha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Tanzania (CCWT), Kusundwa Wamalwa, wakati akizungumza na wafugaji wa Kijiji cha Magungu wilayani hapa kuhusiana na migogoro baina ya makundi hayo.

Wamalwa alisema tathimini iliyofanywa na chama hicho imeonyesha kuwa migogoro hiyo inachangiwa na kamati hizo kushindwa kutimiza wajibu ipasavyo.

"Tathimini inaonyesha kamati hizi hazitekelezi majukumu yao kwa zaidi ya asilimia 75 hivyo kusababisha migogoro ya ardhi kuendelea kuwepo katika maeneo mengi nchini.

"Unakuta wilaya ina mgogoro wa ardhi ambao umedumu kwa muda mrefu lakini hakuna hatua ambazo zimechukuliwa hadi kufikia kuleta machafuko katika eneo husika, "alisema.

Alilitaja tatizo jingine linalochangia migogoro hiyo kuwa ni wafugaji kushidwa kuhudhuria mikutano ya vijiji ambayo imekuwa ikitumika kutunga sheria ndogo na kutoa maamuzi yanalolihusu kundi hilo.

"Wafugaji kuhudhuria mikutano ya vijiji ni jambo la muhimu sana ili mfahamu maamuzi ambayo yamekuwa yakitolewa juu yenu au sheria ambazo zinatungwa ili baadaye mtakapoadhibibiwa kupitia sheria hizo kusiwe na malalamiko," alisema.

Alisema mwaka huu CCWT inatarajia kuhuwisha daftari la wanachama wa chama hicho nchini kwa kuwasajili kwa mfumo wa kidijitali na kuwapatia vitambulisho.

"Nitoe wito kwa wafugaji wote nchini kujisajili katika maeneo yao ili tufahamu idadi yao na mifugo yao na tuweze kuwasaidia katika changamoto wanazokabiliana nazo, " alisema

Kwa mujibu wa Wamalwa, wafugaji ambao watajisajiliwa wapata vitambulisho ambavyo vitawawezesha kupata huduma mbalimbali, ikiwemo msaada wa kisheria, elimu za ufugaji zitakazokuwa zinatolewa katika maeneo yao.

"Tunalenga kuwa na ofisi kila wilaya ili wafugaji wajisajili, pia kupata huduma zote kwa kuwa kila ofisi itakuwa na wanasheria ambao watatumika kutatua migogoro inayowahusu wafugaji, "alisisitiza.



Makamu Mwenyekiti wa chama cha wafugaji (CCWT) Taifa, Wamalwa Kusundwa akizungumza na wafugaji wa kijiji cha Magungu, wilayani Bahi mkoani Dodoma jana, kuhusu utatuzi wa migogoro ya mipaka ya malisho ya mifugo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DC ataka viongozi Dodoma waenziwe

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri ametaka kuwapo na ushirikishwaji wa makundi mbalimbali ili kufanikisha mfumo wa anwani za makazi jijini hapa na majina ya mitaa yawe ya kuenzi historia na viongozi wa Dodoma.

Shekimweri alitoa rai hiyo juzi wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wa mfumo huo maofisa tarafa, watendaji wa kata, wenyeviti na watendaji wa mitaa wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Alisema kuna haja ya kubuni majina yenye upekee badala ya kuwa na jina ambalo linapatikana kwenye mikoa mingine nchini.

"Kuna jina kama Chang'ombe lipo maeneo mengi kuna haja ya kuwa sasa na majina mapya yenye upekee wake. Uwekaji wa vibao vya nyumba na mitaa nipende zoezi liwe la kizalendo zaidi, tunakumbuka mwaka jana tulilumbana kidogo hivi tuliletewa bajeti ya zaidi ya Sh bilioni 10, lakini tukaja na ubunifu na kuondokana na gharama hizo,"alisema.

Aliwataka viongozi hao kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi kwa kuwa anuani za makazi ni hitaji la msingi kwa sasa kutokana na kukua kwa teknolojia.

"Kwa sasa ni rahisi kuita gari la kukodi (Uber) ukaonyesha eneo unapokwenda na huduma hiyo ikakufikia, hivyo hivyo unaweza kuita huduma ukiwa nyumbani kwako," alisema.

Alisema kuna taarifa kwamba mfumo wa anwani za makazi nchini umeleta mafanikio makubwa katika utendaji kazi wa Serikali, ikiwamo ufuatiliaji wa kodi.

"Zoezi hili ni lazima likatekelezwe kutokana na Jiji kukua kwa kasi, makazi yanaongezeka, mitaa inaongezeka hakuna namna zaidi ya kuziingiza taarifa hizi kwenye mifumo yetu.

Zoezi hili ili lifanyike kwa mafanikio ni lazima liwe shirikishi hasa madiwani kwenye mpango kazi muone umuhimu wa kuwashirikisha, " alisema.

Alitoa rai kupitia vikao vya kisheria ikiwamo vya mabaraza ya madiwani kupewa muda wa kuwasilisha elimu na wajibu wao wa kuhamasisha wananchi kujisajili na mfumo wa anwani za makazi.

Awali, Mratibu wa Anwani za Makazi Kitaifa, Jampyon Mbugi, alisema hadi sasa Jiji la Dodoma limekusanya taarifa na kutoa anuani za makazi 245,000, kati ya hizo 163,000 ni za majengo na 81,277 ni viwanja vitupu.

"Wananchi 299,330 ndio waliosajiliwa kwenye mfumo wa anwani za makazi, idadi hii haiakisi uhalisia wa takwimu za idadi watu waliopo ndani ya Jiji la Dodoma inayokadiriwa kuwa zaidi ya 765,000," alisema.

Alisema zaidi ya wananchi 465,849 hawajasajiliwa kwenye mfumo huo na hivyo Serikali imeamua kuongeza msukumo kwa kutumia wenyeviti, watendaji wa kata na mitaa.

"Wizara imeandaa mpango madhubuti wa kuhakikisha taarifa za anwani za makazi zinahuishwa, na mpango unalenga kutumia watendaji wa kata na mitaa na wenyeviti katika kuhamasisha mfumo na kuwezesha upatikanaji wa taarifa sahihi," alisema.

Alisema dhamira ya Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) ni kuhakikisha Dodoma inakuwa ya mfano na kuwa chachu kwa halmashauri nyingine zingine kwenda kujifunza namna ya kufanikisha utekelezaji wa mfumo huo.





# Jamii yatakiwa kuchukua tahadhari Elnino

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameitaka jamii kuchukua hatua ya kuepuka majanga yanayoweza kusababishwa na athari za mabadiliko ya tabia nchi na mvua za elnino zinazotarajiwa kunyesha nchini.

Othman alitoa tahadhari hiyo katika Shehia ya Mtoni Chemchem, Jimbo la Mwera, Wilaya ya Magharibi A Unguja wakati wa ziara ya kukagua maeneo yaliyokumbwa na athari za kimazingira kutokana na mabadiliko hayo ya tabianchi.

Alisema jamii na Taifa linatakiwa kuchukua tahadhari ya kukabiliana na maafa kutokana na mitaro isiyokuwa salama, hasa kwa wakati huu ambao Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) imetoa taarifa ya kuwepo kwa tishio la elnino nchini baadaye mwaka huu.

Othman, alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) , itahakikisha mazingira na maisha ya wananchi yanakuwa salama kwa kuimarisha miundombinu.

Aliuagiza uongozi wa jimbo hilo, kufanyakazi kwa ushirikiano na mamlaka za wilaya, shehia na jamii za Mtoni Chemchem ili kulinda mazingira na wananchi dhidi ya maafa yanayoweza kuepukika kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Awali Mkuu wa Wilaya ya Magharibi A Unguja, Suzane Peter Kunambi, alitoa wito kwa jamii kwa kuitaka kubadilika kwa kutunza mazingira na kuyaweka katika hali ya usafi. Alisema kufuatia ziara hiyo, uongozi wake umeanzisha Programu Maalum ya Usafi, ukiwemo wa kusafisha mitaro na kuomba ushirikiano kwa wananchi ili kufanikisha mpango huo.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mazingira, Sheha Mjaja Juma, aliwataka wananchi kuepuka kujenga makazi katika maeneo hatarishi ili kuepuka maafa yanayoweza kusababishwa na mabadiliko hayo ya tabianchi.

# Funza watibua soko la embe kimataifa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Shamata Khamis amesema wizara yake inaendelea na utafiti wa wadudu waharibifu wa mazao ikiwamo nzi baada ya kuharibu soko la embe kimataifa.

Khamis aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Ali Ameir aliyetaka kujua juhudi zinazofanywa na wizara yake kupambana na wadudu wanaoshambulia mazao ya wakulima mashambani na kukwamisha juhudi zao kujiletea maendeleo.

Alisema kuanzia mwaka 1990 wamejitokeza wadudu wanaoshambulia mazao ya wakulima, ikiwemo matunda aina ya embe na machungwa na hivyo kurudisha nyuma juhudi zao katika maendeleo ya kilimo na uzalishaji wa mazao. Alisema nzi hao wamesababisha hasara kubwa kwa wakulima kuacha kusafirisha mazao nje ya nchi baada ya wanunuzi kupiga marufuku uingizwaji wa embe.

"Wakulima wa embe waliokuwa wakisafirisha bidhaa hizo nje ya nchi wamesita kufanya hivyo kwa sababu ya mazao hayo kushambuliwa na nzi ambao huzalisha mafunza," alisema.

Akifafanua zaidi alisema kituo cha utafiti wa mazao ya kilimo kilichopo Kizimbani kinaendelea kufanya utafiti kwa kushirikiana na taasisi za kimataifa ikiwemo ya Ujerumani.

Waziri huyo alisema taasisi hizo zimelenga kufanya utafiti wa mazao ya kilimo na mifugo na kufahamu sababu za kuwepo kwa nzi hao.

"Tumetiliana saini na taasisi ya mifugo na mazao ya Ujerumani kwa ajili ya kufanya kazi za utafiti zitakazohusisha wadudu wanaoshambulia mazao ya wakulima na kurudisha nyuma uzalishaji, " alisema. Alisema wakulima wa embe aina ya Boribo katika kijiji cha Muyuni mkoa wa kusini Unguja wamesitisha usafirishaji wa mazao yao baada ya nzi kuzalisha funza na kukosa sifa katika Soko la Kimataifa.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kulia), akitoa maelekezo mbele ya viongozi mbalimbali, alipowasili huko Shehia ya Mtoni Chemchem, Jimbo la Mwera, Wilaya ya Magharib A Unguja juzi, kwaajili ya kukagua daraja linalojengwa, jirani na mtaro ambao ni tishio la mafuriko, nyakati za mvua. **PICHA: OMKRZ**

# SMZ kukarabati nyumba ya jaji Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) inatarajia kuifanyia ukarabati nyumba ya Jaji Mkazi Pemba na kuweka samani mpya katika mwaka wa fedha wa 2023/24.

Mpango huo ulitangazwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba na Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Suleiman alisema nyumba hiyo itakarabatiwa na kuwa na hadhi, kisha kuwekewa thamani katika robo ya pili ya bajeti.

Akiwasilisha mapendekezo ya Kamati ya baraza hilo ya viongozi wakuu wa kitaifa kuhusu mapendekezo ya utekelezaji wa kazi zake, alisema Serikali pamoja na mambo mengine, imetekeleza miongoni mwa malalamiko ya wajumbe wa baraza hilo zaidi waliokuwa wakitoka Pemba ya kutaka kuwepo kwa Jaji Mkazi ambaye atashughulikia haraka kesi ambazo zitatolewa maamuzi ngazi ya majaji.

Alisema Jaji Mkazi yupo wa Pemba na ameanza kutekeleza majukumu yake na kupunguza malalamiko ya wananchi ya kucheleweshwa kusikilizwa kesi zao na kutolewa maamuzi katika ngazi ya juu.

"Mheshimiwa Spika niwaambie wajumbe wa baraza la wawakilishi kwamba Jaji Mkazi ameanza kutekeleza majukumu yake Pemba hatua ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza na malalamiko yaliyokuwepo ngazi za Mahakama Kuu na kuyatolea maamuzi, " alisema.

Akichangia bajeti hiyo, Mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Professa Omar Faki Hamad alisema kuwepo kwa Jaji Mkazi Pemba kumerudisha imani ya wananchi kutimiza malengo ya utawala bora na haki jinai.



**AKON**

UKURASA 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI SEPTEMBA 16, 2023



# REMA KAWA SOMO wasanii BongoFleva

WAKATI wasanii wa bongo Fleva,wakiwa katika wingu zito la ufahamu na kubaki wakitafuta kiki zisizo na maana, wenzao kule Nigeria, wanaendelea kupambana kupenya katika soko la muziki la Marekani.

Muziki wa Bongo Fleva licha ya kukua kwa kiasi fulani, lakini umeanza kupoteza mwelekeo kutokana na wasanii wenyewe kukosa kutambua jukumu lao la msingi la kuukuza na kuotesha mizizi kila kona ya dunia.

Hivi sasa mwanamuziki wa Nigeria, Divine Ikubor, almaarufu Rema, ambaye huko nyuma alikuwa yuko nyuma ya Diamond kwa umaarufu, ameaza kuchomoka kwa kasi baada ya kuanza kufanya kazi na wasanii wakubwa wa Marekani.

Rema sasa anataka kufanya kolabo na mastaa wengine maarufu wa Marekani ili kutimiza malengo yake, baada ya kupata mafanikio baada ya wimbo wake mkali na Selena Gomez, unaoitwa 'Calm Down kutikisa dunia.

Msanii huyo mzaliwa wa Benin amesema anataka kufanya kazi na mastaa wa kike kama Nicki Minaj na Megan Thee Stallion.

Kutokana na kuweka nguvu zote katika mipango yake ya kupanda juu, iko siku Rema tutamsikia amekuwa namba ya juu, huku wasanii wetu wakiendelea kulala na kulewa mafanikio madogo waliyopata.

Rema aliwashinda Wizkid, Davido, Burna Boy na wengine na kuwa mshindi wa kwanza wa wimbo mpya bora wa Kiafrika wakati wa Tuzo za Muziki za MTV.

Wanamuziki kama Ali Kiba, Harmonize, Nandy na Zuchu waone kinachofanywa na Rema kama somo kwao kwani majivuno na kujitapa kwa kufanya kolabo na wasanii wa Nigeria sasa imepitwa na wakati, badala yake tunataka kusikia wanavuka mipaka ya Afrika kwa kufanya kazi na wakali wa Marekani kama ilivyo kwa wenzao.

## BASI SAWA



## Shusho kuitikisa Kenya

MWIMBAJI wa muziki wa Injili, Christina Shusho, yuko nchini Kenya kwa mwaliko maalum wa mchekeshaji maarufu Eric Omondi.

Shusho akiwa nchini humo ataimba katika matamasha mbalimbali ambayo yameandaliwa kwa ajili ya kurejesha muziki wa injili ambao unaendelea kuyumba nchini humo.

Shusho aliwasifia waimbaji wa Kenya kwa kuwaelezea kwamba wanafanya vyema japo kuna mapungufu.

Aliwataja baadhi waimbaj hao kuwa Mercy Masika, Daddy Owen na Gardian Angel.

## Huyu ndiye Y Prince



MSANII chipukizi wa Bongo Fleva, Y Prince amesema wazo la kuimba wimbo wa Msukule ni kutokana na maisha ya kila siku ya mtaani.

Wimbo huo wa Y Prince akishirikisha na Founder Tz, unafanya vizuri katika mtandao wa Youtube na kushika nafasi ya kumi bora.

"Nawashukuru Watanzania kwa kukubali kazi zangu, safari yangu imeanza na natarajia wataendelea kuniunga mkono wakati wote," amesema Y Prince.



## HAMISA SI HABA MAMA

MWANAMITINDO na mwanamuziki wa Bongo Fleva, Hamisa Mobetto urembo wake unatokana na mwili wa asili na usiochafuliwa na maisha ya kisasa.

Mobetto kupitia ukurasa wake wa Instagram, aliweka wazi kwamba hakuna michoro yoyote kwenye mwili wake na wala hajafanya upasuaji wa kuongeza mwonekano.

"Mimi sina tattoo hata moja kwenye mwili wangu, sipendi tu lakini napenda kuziona kwenye miili ya watu lakini sio kwangu. Pia mimi sijawahi kufanya upasuaji wowote kwenye uso wangu. Si mnaona uso wangu ulivyo kama nilivyozaliwa, hakuna uboreshaji wa sajari,"amesema.



## Ben Pol ajilegeza kwa warembo

MKALI wa muziki wa R&B nchini, Ben Pol, amesema imefikia wakati hawezi kuwa na vigezo kwa mwanamke anayetaka kuwa naye.

Ben Pol amesema huko nyuma alikuwa na vigezo vingi hadi anamkubali mwanamke ambaye alikuwa naye katika mahusiano ya kimapenzi, lakini kwa sasa mambo mengi yamebadilika.

"Siwezi kuwa na vigezo kwa sasa, kila mwanamke ambaye naona ananifaa naweza kuingia naye katika uhusiano. Mimi ni mtu wa kuheshimu kila mtu na hata mwanamke nataka awe hivyo ila sitaki kusema awe na umbo hili au maisha haya," amesema Ben Pol.

## FILAMU

# Adui ndani ya: Mwema ndiyo mbaya wako

**Na Adam Fungamwango**

UMESHAWAHI kuitazama filamu ya 'Adui Ndani Ya...?' Mtunzi alitaka ujumbe wake uwaendee walimwengu, ili wajue jinsi gani ya kuishi na watu duniani.

Dunia ni uwanja wa kupita tu. Haifai watu kutendeana ubaya. Ni filamu iliyochezwa na baadhi ya wasanii maarufu mama Hashim Kambi, Nisha, Flora Mvugi, Fadhili Maogola, Rashid Jabu, Makiragi Makiragi, Mzee Ulaiti, Justice Musiba, Latifa Issa, Robert Mlambala na wengine.

Inaanza kwa kumuonyesha msichana mdogo wa darasa la tatu hivi akiingia ndani kwao kutoka shule. Lakini anakuta baba yake amenyong'wa sebuleni. Anaingia chumbani, mama, kaka na dada yake wako chini ya ulinzi wa mzee Kambi na baadaye kuuawa. Kilichotokea ni kwamba na yeye anachukuliwa mzobemzobe pamoja na miili ya wazazi wake na wanaenda kutupwa porini. Walijua na yeye pia anaweza kuliwa na wanyama wakali. Haikuwa hivyo. Msichana huyo Linda, anaokotwa na wanakijiji cha jirani. Mzee Ulaiti anajitolea kumtunza, licha ya kupata upinzani mkali kutoka kwa mkewe na mabinti zake wawili. Mkewe inafikia wakati anahisi kuwa huenda ni mtoto wa nyumba ndogo kwa jinsi alivyompenda.

Miaka 10 baadaye, mzee kambi anampokea kijana wake Tonny aliyetoka Ulaya kwa masomo. Siku chache baadaye anapata ajali ya gari. Gari lake inaungua. Mzee Kambi na mkewe wanadhani amefariki. Lakini Tonny alijikokota porini na kwenda kuishia kwenye kijiji alicho Linda.

Anapokewa na mzee Ulaiti ambaye anampa chaguo la kuchagua msichana na kurejea naye mjini, pale atakapopona kabisa. Anamchagua Linda kati ya mabinti watatu. Hata hivyo Linda wakati huo ameshakuwa kiziwi na bubu kutokana na kadhia aliyoipitia, akishuhudia wazazi wake wakiuawa.

Hata hivyo haikuwa shida kwa Tonny. Alipopona akamchukua hadi mjini. Linda akakumbuka kila kitu, kuwa ameletwa kwenye familia ambayo iliwaua wazazi wake.

Dunia haina siri, Mzee Kambi na mkewe anakuja kugundua kuwa msichana aliyeletwa na kijana wao ndiyo yule ambaye zaidi ya miaka 10 iliyopita waliwaua wazazi wake.

Juhudi za kutaka kumuua zilishindikana kutokana na Tonny na dada yake Loveness kusimama imara kumlinda Linda. Wauaji wa kukodishwa wanashindwa na Mzee Kambi na mkewe wanauawa.



# KING GEOVANI MFALME WA MDUARA

**Na Adam Fungamwango**

ILIKUWA ni ngumu kwa mashabiki wa muziki wa dansi nchini Tanzania, baada ya kutangazwa habari za kifo cha mwanamuziki mahiri wa Chuchu Sound, King Geovani.

Mwanamuziki huyo ambaye ni mpiga solo, alifariki ghafla Aprili 5, 2021 baada ya kupatwa na shinikizo la damu kwa mujibu wa mwanamuziki mwenzake, King Dodoo.

Mwanamuziki mpiga gitaa ongozi la solo alifariki siku chache baada ya kurekodi wimbo wa kumlilia aliyekuwa Rais wa Tano wa Tanzania, John Magufuli Machi 17 mwaka huo.

King Geovani, mwenye asili ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo alipata umaarufu sana mwanzoni mwa miaka ya 2000 alipojiunga na Chuchu Sound, bendi ndogo ambayo ilitikisa nchi kwa nyimbo zake kali, zikiwemo zile za mduara, huku nyingi yeye alipiga gitaa ongozi la solo.

Akiwa na mmiliki na kiongozi wa bendi hiyo,Yusuph Chuchu, Mao Santiago, Gabby Katanga ambao wote ni marehemu, kukiwa pia na Jenico Flower pamoja na Omari Mkali, walitengeneza bendi iliyozikisa vigogo.

Leo tunamkumbuka na kuzienzi kazi zake tano alizozifanya, akipiga solo kwenye nyimbo za mduara.

**Sitishiki**

"Sitishiki mimi sibabaiki, niko freshi na niko fiti...Si kwa mzizi si hirizi jambo lilo huwezi...si rahisi kuchota maji kwa pakacha kuliko yeye kuniacha..." Hayo ni baadhi ya maneno kwenye wimbo huo.

Hizi ni baadhi ya nyimbo za mwanzo kabisa zilizoanza kuipa umaarufu bendi hiyo. Upo kwenye mtindo wa mduara. Utamu wa nyimbo hizi huchagizwa na sauti ya Omari Mkali kwenye vibwagizo, lakini pia linapoachia solo la marehemu, Mkali hupagawa na kuita kwa sauti "King Geovaniii."

**Marafiki**

Huu ni moja ya nyimbo chache za Chuchu ambazo hazipo kwenye mtindo mduara lakini zikapata umaarufu mkubwa.

Chuchu walikuwa wakichanganya nyimbo za mitindo mbalimbali, lakini zile za mduara kwa kiasi kikubwa ndizo zilizofanya vizuri. 'Marafiki' ni wimbo ambao haukuwa na mduara, lakini solo la King Geovani na sauti tamu ya Jenico Flower ulifanya wimbo huo kupendwa sana.

**Hodi hodi**

"Hodi hodi, wana Chuchu ooo, twaingia tena 2001." Ilikuwa ni albamu nyingine ya pili waliyoingia nayo ambayo walitaka kuthibitisha kuwa ile ya kwanza hawakubahatisha. Na kweli, ikashika vilivyo. Baada ya hapo Chuchu Sound ikawa ni bendi tishio na yenye mashabiki wengi kila kona ya nchi. Geovani naye alionekana pia ni hatari kwa wapiga solo wengine.

**Usione Vyaelea**

Wimbo huu ni mfululizo wa nyimbo za mduara ambazo walikuwa wakizitoa Chuchu Sound na kufanya vema mno. Hakuna tena mashabiki aliokuwa na wasiwasi nao. King Geovani naye alizidi kuonyesha ufundi wake kiasi cha bendi nyingi kumtamani.

**Shanuo**

Ni wimbo mkali wa mduara ambao nao ulitikisa hasa. Kwa bahati mbaya sana wimbo huu ni moja kati ya zile za mwisho wa uhai wa bendi hii, kwani pamoja na yote ulirekodiwa wakati baadhi ya wanamuziki wake wakiwa wameshaanza kusambaratika kwa kuchukuliwa na bendi zingine. King Geovani yeye alikuwepo na kupiga solo kama kawaida.

"Salama ni salama wala sina gharama, kutenda mtende nyie, tukitenda siye lawama." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo.




## Rema, Selena hawakamatiki

MSANII wa muziki kutoka Nigeria, Rema na nyota wa pop wa Marekani Selena Gomez, wameshinda Tuzo za Muziki wa Video za MTV 2023.

Wawili hao walitwaa tuzo hiyo katika kipengele cha muziki bora wa Afrobeats kwa kibao chao kikali “Calm Down.”

Wimbo huo ulishindanishwa na vibao vingine kama “Rush” ya Ayra Starr, “It’s Plenty” ya Burna Boy na Davido.



## Joe Jonas talaka yamchanganya

MWANAMUZIKI nyota wa Pop nchini Marekani, Joe Jonas, anaonekana kunyamazia suala la kuachana na mkewe Sophie Turner na akawataka mashabiki wake kutoamini kile wanachosikia.

Jonas akiwa katika ziara yake ya kimuziki huko Los Angeles, alikuwa mwenye hisia kali wakati akiimba wimbo wa Hesitate kutoka kwa albamu yao ya 2019 ya Happiness Begins.

“Imekuwa wiki ya mambo, nataka tu kusema, ikiwa husikii kutoka kwa midomo hii, usiamini. Sawa? Asante kila mtu kwa upendo na msaada wako. Mimi na familia yangu tunakupenda.” Aliwaambia mashabiki wake.

## Kourtney mama kijacho

MWANAMITINDO Kourtney Kardashian, amethibitisha kuwa ana ujauzito na kwamba hivi karibuni alikwenda hospitali kuchunguza afya yake na mtoto.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, amebainisha kuwa alifanyiwa upasuaji mdogo na alitoa shukrani zake kwa madaktari wake kwa kuokoa maisha ya mtoto wake ambaye hajazaliwa.

Aliweka picha nyeusi na nyeupe akiwa kitandani hospitalini akiwa amemshika mkono mumewe Travis Barker.





## Kumbe Akon mkono chuma

MWIMBAJI maarufu wa Marekani ambaye ana asili ya Senegal, Akon, amejitambulisha kama mtu mbahili zaidi duniani.

Kulingana na Akon njia bora ya mtu kubaki tajiri lazima awe na matumizi sahihi ya kipato chake.

“Mtu bahili zaidi kwenye sayari, ndio ufunguo wa kudumisha utajiri, amesema.

## Genevieve arudi kivingine

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Genevieve Nnaji, hatimaye amerejea kwenye mitandao ya kijamii baada ya kufuta ukurasa wake wa Instagram miezi kadhaa iliyopita.

Mashabiki wa msanii huyo na mtayarishaji wa filamu walivamia ukurasa wake baada ya kuweka chapisho lake la kwanza na picha kadhaa za onyesho la kwanza la filamu yake ya ‘I Do Not Come To You By Chance’. Genevieve aliweka picha za tofauti zilizopigwa kwenye zulia jekundu la tukio na mambo mengine katika onyesho lake la kwanza la sinema.



HABARI KASKAZINI

## Wizara yawakutanisha madaktari bingwa

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

WIZARA ya Afya, imeanza kwa kasi utekelezaji wa vipaumbele vyake 14 vya bajeti, kwa kuwakutanisha madaktari bingwa, waganga wafawidhi wa hospitali za rufani za mikoa, makatibu wa hospitali na maofisa utumishi, kuweka mipango na uelewa wa pamoja wa namna ya kuvitekeleza kwa tija katika mwaka wa fedha 2023/2024.

Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Tiba, anayesimamia utoaji huduma katika hospitali za umma na za binafsi nchini, Dk. Caroline Damian, alisema wamelazimika kuandaa kikao kazi hicho maalum kwa ajili ya usimamizi wa hospitali za rufani za mikoa, kuvipitia vipaumbele hivyo na kuvitekeleza kwa ufanisi na tija kubwa.

Alikuwa akizungumza jana Jijini Arusha katika kikao kazi cha siku tatu cha wataalam wa wizara hiyo.

Wataalam hao, pamoja na mambo mengine, walipata fursa ya kuupitia mradi wa kuimarisha huduma za mama na watoto wachanga katika hospitali za rufani za mikoa.

Mradi huo wa miaka mitano (2022/2026) wa kuimarisha huduma za mama na watoto wachanga katika hospitali za rufani za mikoa, unatekelezwa na serikali ya Tanzania, kwa ushirikiano na Shirika la Maendeleo la Japan (JIKA).

"Tumeandaa kikao kazi hiki kwa ajili ya usimamizi wa hospitali za rufani za mikoa, kupitia vipaumbele vya sekta ya afya kwa mwaka wa fedha 2023/24.

"Wizara ina vipaumbele vingi lakini mahususi kwa mwaka huu wa fedha, tuna vipaumbele 14. Sasa katika utekelezaji wake kuna vile ambavyo utekelezaji wake unahusisha moja kwa moja hospitali zetu za rufani, ambazo zinatoa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi.

...Kimuundo hizi hospitali za rufani za mikoa zinatakiwa kutoa huduma za kibingwa; kwa hiyo kipaumbele kimojawapo ni kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi."

Kwa mujibu wa Dk. Caroline, kutokana na uwekezaji mkubwa wa miundombinu, kwa maana ya watumishi wenye weledi, wao kama wataalam inabidi waonyeshe kwa vitendo Watanzania, uwekezaji uliofanyika unaendana na huduma wanazozipata katika hospitali hizo



Mwenyekiti wa viongozi wa mila wa jamii ya kifugaji ya Kimaasai, Kata ya Donyomoruwa, Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, Dickson Mollel (kulia), akizungumza katika mkutano mkuu wa kijiji cha Oloiwang, kabla ya kupitishwa sheria ndogo ya kupinga ukeketaji, kuozesha watoto, mimba za utotoni na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

## Wanakijiji wapitisha sheria wanaoozesha watoto

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WANANCHI wa Kijiji cha Loiwang' kilichoko Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, wamepitisha sheria ndogo inayong'ata zaidi familia za kifugaji zinazopokea 'sukari' kwa ajili ya kuozesha watoto wenye umri mdogo, kupinga masuala ya ukeketaji na ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

Sheria hiyo imeweka adhabu ya Sh.100,000 ama kifungo cha miezi mitatu au vyote kwa pamoja kwa atakayepokea sukari ili mwanaye aolewe.

Akizungumza jana kijijini humo, kabla ya mkutano mkuu wa kijiji kupitishwa sheria hiyo kali ya kuwabana wanaoendeleza vitendo hivyo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Loiwang' kilichoko Kata ya Donyomoruwa, Joseph Kivuyo, alisema wamefikia uamuzi huo kutokana na Kijiji chao kutishiwa na ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto.

"Tunakwenda kupitisha sheria hii ili mtu yeyote atakayemkeketa mtoto wa kike tumchukulie hatua za kisheria kwa kushirikiana na vyombo vya dola. Tutaendelea pia kutoa elimu kwa mangariba waache kabisa biashara ya kukeketa wasichana na watoto.

"Kwenye ndoa za utotoni, tumesema mtu yeyote atakayechukuwa sukari au kupokea posa, kama kijiji kabla ya vyote tutampiga faini ya shilingi 100,000 ama kifungo cha miezi mitatu jela au vyote kwa pamoja kwa kosa la kupokea sukari au posa." Aidha, Katibu wa viongozi wa mila (Malaigwanani) wa jamii ya kifugaji ya Kimasai, Kata ya Donyomoruwa, Luka Mollel, alisema wao kama viongozi wa mila wameamua nao waielimishe jamii yao kuachana na vitendo hivyo ambavyo ni kinyume na haki za binadamu.

"Malaigwanani tumekubaliana kwamba vijiji vyetu vije na sheria hii kwa sababu tumeona umuhimu wa elimu. Sasa tunataka waachane na mila za kuozesha watoto na wawapeleke shule.

...Kwamba hata ukeketaji sasa basi katika vijiji vyetu.tunaona mtu amesomesha mtoto lakini anarudi nyumbani ana mimba kapewa na kijana.Huko ni kukatis

Katika mkutano huo, Mwanasheria wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Alfred Joshua, alisema vijiji vinne ambavyo vinakaliwa na idadi kubwa ya wafugaji wa Kimasai vilivyopitisha sheria ndogo, ni Embukoi, Donyomoruwa, Munge na Loiwang'. Wakati, Mkuu wa Divisheni ya Maendeleo ya Jamii ya Wilaya hiyo, Marko Masue, alisema: "Kama serikali hatutakuwa na kikwazo katika hili, kwa sababu ni hitaji la jamii yenyewe. Imeamua kukemea, kupinga ukeketaji, ndoa za utotoni, kuozesha watoto na vitendo vyovyote vya ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto.

"Tunawashukuru wadau wa maendeleo, hasa washirika wetu ambao wametusaidia kufikia mafanikio haya, Shirika la KWIECO na wafadhili wao FNF (Friedrich Naumann Foundation Tanzania)."

Kwenye mkutano huo, Ofisa Mradi wa Haki za Binadamu Pamoja na Jinsia kutoka Shirika la KWIECO, Elizabeth Mushi, alisema wanafanya kazi ya kuzijengea uwezo jamii za kifugaji Wilayani humo, kupinga vitendo hivyo kupitia mradi wa jamii salama.

Kwa mujibu wa Elizabeth, lengo la mradi huo ni kuwaokoa wanawake na watoto wanaokabiliwa na ukatili wa kijinsia, ambapo kwa mwaka huu, tayari wamefanikiwa kuwapa mafunzo Malaigwanani 48, mangariba na baadhi ya watu katika vijiji hivyo, wakiwamo wanawake wa Kimasai.

## EWURA yataka wafanyabiashara wa mafuta kuingia mikataba

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji nchini (EWURA), imesema njia pekee ya wafanyabiashara wa mafuta ya dizeli na petroli, kukabiliana na uhaba wa nishati hiyo kila mara, ni kuingia mikataba na waagizaji wakubwa wa mafuta.

Jana, Meneja wa EWURA, Kanda ya Kaskazini, Lorivu Lon'gidu, alisema mikataba hiyo ni suluhisho la vitu vingi kukosa mafuta, kwa kuwa itaondoa mateso hayo na kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta katika vituo vyao.

Long'idu alikuwa akizungumza na wafanyabiashara binafsi wa mafuta katika kikao kazi kilichoandaliwa na EWURA na kufanyika jijini Arusha. "Kiujumla kikao kazi hiki, lengo lake ni kukumbushana taratibu za ufanyaji biashara ya uuzaji wa mafuta. Hapa tumekutana wafanyabiashara wa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga.

"Mnao wajibu wa kutoa huduma za kuwauzia wananchi mafuta bila kubagua, kwa kufuata taratibu na sheria. Kuna baadhi ya wafanyabiashara, wamekuwa hawafuati taratibu na sheria za ufanyaji biashara ya mafuta .

...Sasa hili tatizo la kukosekana mafuta kwenye vituo, EWURA tunashauri ingieni mikataba na waagizaji mafuta nchini. Lengo la mikataba hii nini nini ? unakuwa na uhakika wa upatikanaji wa mafuta.

Sababu hawa waagizaji wakubwa wa mafuta, wanatabia moja; unapoagiza mafuta, lazima wajue hayo mafuta wanamuuzia nani. Kuna ambao wana mikataba, lakini kuna ambao hawana mikataba, na wengi wao ndio wanakosa mafuta na kuanza kulalamika."

Hata hivyo, baadhi ya wafanyabiashara wa mafuta akiwamo, Marco Masanja kutoka Mkoa wa Tanga, alisema baadhi yao wana mikataba na wafanyabiashara hao wakubwa, lakini wekuwa wakikosa huduma ya mafuta.

Masanja, alisema kuna mchezo mchafu unaendelea kati yao na waagizaji, ambao huwasumbua kupata mafuta hayo na wengine wakiambiwa walipe fedha mara mbili.

"Unakuta mimi nimelipia mafuta leo kwa uyo mfanyabiashara mkubwa na nina mkataba lakini cha kushangaza nikitaka mafuta nazungushwa, muda mwingine naambiwa niongezee fedha mafuta yamepanda lazivyo nirudishiwe fedha au unakuta kuna mtu anataka nitoe cha juu ili nipate ukiangalia kituo changu cha mafuta akina mafuta ,mkuu wa mkoa anakuja anajua nimeficha mafuta ,toyo ambazo ndio wateja wetu wakubwa wanakuja wanataka kunitoa roho, "alisema Masanja

Kutokana na hali hiyo, wafanyabiashara hao wameitaka EWURA kukaa na wafanyabiashara wakubwa wanaoagiza mafuta na kupanga bei ambayo itakuwa hamnyimi faida muagizaji.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

## MIAKA 45 YA SIKINDE...

# Bendi iliyoanzishwa kama masihara, kupanda jukwaani ikapagawisha balaa!

**Na Adam Fungamwango**



Mwimbaji tegemeo wa bendi ya Orchestra Mlimani Park, Hassan Rehani Bitchuka kushoto na mpiga gitaa la solo, Henry Mkanyia wakiwajibika jukwaani.




Michel Bilal, mpiga gita la solo kulia na Abdallah Gama mpiga gita la kati, rhythm gitaa, wakitumbiza mashabiki kwenye moja ya kumbi ambazo bendi hiyo ilikuwa ikipiga na picha hii ilipigwa katikati ya miaka ya 1980.

WAZEE hawajakosea hata siku moja, jambo lolote huanza na wazo. Uongozi wa Ukumbi wa Mlimani Park ambao sasa unabomolewa, pale jirani na Mlimani City, Dar es Salaam, walianza kwa kuikaribisha bendi ya Dar International kwenye mahafali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Baada ya kuwashuhudia walivyotimia kikazi, wanavyoporomosha muziki na kushambulia jukwaa, huku umma ukiwa umepagawa kwa furaha, wakafikia uamuzi kuwa 'hawa hawa ndiyo wanatufaa', maana waliokuwa wamelenga awali, bendi ya Kizaire (sasa DRC), Orchestra Fukafuka walikuwa wanamaliza mkataba na hawana mpango wa kubaki Tanzania.

Naam! Upande wa ukumbi wa Mlimani Park, mzee Mwangama na washika magitaa wa Dar International wakiongozwa na bwana mipango, Abel Barthazar, wakateta jambo lao, wakaingia mkataba, mtoto Orchestra Mlimani Park akazaliwa.

### ILIVYOUDWA RASMI

Kwa lugha fupi, ile Dar International ambayo ni mpya kwenye plastiki begi yake, wakiwa wamerekodi nyimbo sita tu Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), wakahamishwa kama walivyo, isipokuwa mabinamu wachache kama Beresa Kakere, Kassim Mponda, fundi mitambo Athumani Michuzi, na Marijani Rajab ambaye alikuwa amesimamishwa, wakaachwa kwa staili ya mtajijua.

Hapa ina maana kama Marijani angekuwa hajasimamishwa, basi naye leo hii angekuwa kwenye historia ya kuipigia bendi ya Mlimani Park Orchestra.

Mtaani wakati huo, ambao King Kiki aliuita Dar es Salaam inachemka kama bahari kwa dansi lilivyonoga ukazua mjadala kila kona hadi kwa watoto wa shule za msingi, 'bendi kubwa imeanzishwa...

Hilo ni tukio la Agosti Mosi mwaka 1978, ambalo mpaka sasa lina miaka 45.

Hawakupata tabu kulipata jina, kwani pale pale walipokutania na kutolewa wazo hilo, Ukumbi wa Mlimani, jina likaamuliwa liwe hilo hilo. Ikaitwa Orchestra Mlimani Park.

Kama nilivyosema awali kuwa ilikuwa na wanamuziki wote wa Dar International kasoro wale niliowataja, lakini mastaa hasa walikuwa ni Bathazar ambaye alikuwa kiongozi wa bendi, Abdallah Gama, Cosmas Thobias Chidumule, Joseph Mulenga na Michael Enock.

Walipokaa wenyewe wakaona bado hawajakamilika, wanamfuata mwimbaji wa sauti ya kwanza Hamisi Juma 'Maalim Kinyasi' ambaye walishawahi kuwa naye kwenye bendi ya Dar International kipindi fulani kabla ya kwenda Biashara Jazz. Naye akajumuika.

Kama vile haitoshi wakaenda kung'oa Muhidini Maalim Gurumo katika bendi ya Juwata Jazz 'Msondo Ngoma', na kumjumuisha kwenye kundi.

Gurumo ndiye aliyeleta jina la mtindo wa bendi mara baada ya kuingia, ikaitwa 'Sikinde Ngoma ya Ukae', ikiwa ni moja kati ya ngoma za asili ya kwao, Uzaramoni.

Baada ya kutoa albamu mmoja tu ambayo iliteka nyoyo za mashabiki wa muziki wa dansi nchini, iliyokuwa na vibao kama 'Selina', 'Maudhi', 'Weekend na Sikinde' na vingine, wakaka haistoshi.

Wakarudi tena Msondo na kuwachukua mwimbaji wa sauti ya kwanza Hassan Rahani Bitchuka, Suleiman Mwanyiro ambaye ni mpiga gita la besi na Hassan Juma 'Town', mpuliza saxophone, kikosi kikawa kimekamilika.

Wamiliki wa kwanza wa bendi hiyo walikuwa Chama cha Madereva Taxi, Tanzania Transport & Taxi Services (TTTS), ingawa kulikuwa na minong'ono mitaani kuwa hapo ni kama iliegemezwa tu, lakini ilikuwa ikimilikiwa na moja kati ya idara nyeti nchini.

Mwaka 1982 iliondoka kwenye umiliki wa TTTS na kukabidhiwa Shirika la Maendelea Mkoani Dar es Salaam, Dar es Salaam Development Corporation (DDC).

Hapo sasa ikaachwa kuitwa Orchestra Mlimani Park, ikaanza kuitwa DDC Mlimani Palr Orchestra lakini kila kitu kikabaki pale pale.

### TIMU YA TAIFA, MABINGWA WA MUZIKI

Kadri siku zilivyozidi kwenda bendi hiyo ilikuwa ikipata wafuasi na wapenzi wengi kutokana na vibao vyao vingi bora kuanzia kwenye uimbaji hadi upigaji.

Japo ilianzishwa mwaka 1978 ikikuta bendi nyingi, lakini ilikuwa tishio na kuziacha bendi nyingi nchini kwa umaarufu, ubora na kupendwa na mashabiki wengi, isipokuwa Juwata Jazz Band tu.

Hapo sasa ukaanza upinzani wa jadi katika ya makundi hayo mawili, na uhasama ulikuwa mkubwa sana kati ya bendi hizo mbili na mashabiki wake kutokana na zote kupiga muziki wa kiwango cha juu, lakini Sikinde ikiwa inazoa wanamuziki kutoka Msondo kila inavyojisikia kufanya hivyo.

Kitu hicho kilikuwa kinamkera sana mzee Gurumo japo alikuwa yupo Sikinde, lakini hakutaka bendi ya Msondo itetereke au ife kwa sababu yeye ni mmoja kati ya wanamuziki wa mwanzo wa bendi hiyo, akiipa jina la mtindo wa 'Msondo Ngoma' ambayo pia ni ngoma ya Kizaramo.

Kabla hajafariki aliwahi kunukuliwa kuwa lengo la viongozi wa Sikinde ni kuiua Msondo na yeye hakutaka hivyo kwa sababu zote mbili ni bendi zake.

Hadi leo hii bendi hizo zimebaki wa ushindani kama ule wa Simba na Yanga na ndizo zimebaki wa mashabiki wengi kuliko zote zingine za muziki wa dansi.

Baada ya kutoa albam nyingi zikapendwa na kile wimbo ukachoma kwenye mioyo ya mashabiki, bendi hiyo ikafananishwa na timu ya taifa, Taifa Stars wakati huo kutokana na kusheheni pia wanamuziki nyota na wenye uwezo mkubwa.

Na wala haikushangaza ilipotwaa Ubingwa wa Muziki Tanzania katikati ya miaka ya 1980.

### SHEREHE ZA KUTIMIZA MIAKA 45

Tarehe 30 mwezi huu, bendi hiyo inatimiza miaka 45, huku kukiwa kumeandaliwa bonge la sherehe, pamoja na onyesho kabambe.

Onyesho hilo litafanyika kwenye moja kati ya kumbi zake zilizokuwa zinavuma sana na maarufu, DDC Magomeni Kondoa, jijini Dar es Salaam.

Wamiliki wa bendi hiyo walikuwa wakilipia kumbi hiyo, ikiwemo DDC Kariakoo na DDC Keko.

Kwa bahati nzuri wamiliki wa zamani wa bendi, Shirika la Maendeleo Dar es Dalaam, DDC limeamua kushirikiana na bendi hiyo kwa ajili ya sherehe hiyo.

Pamoja na kwamba kwa sasa bendi hiyo inamilikiwa na wanamuziki wenyewe, lakini wameamua kuanzia sasa kuingia makubaliano na kuifadhili kwenye baadhi ya maeneo.

Hiyo ndiyo Mlimali Park Orchestra, moja ya bendi kubwa nchini Tanzania.




Basi aina la Leyland lililokuwa linatumiwa na wanamuziki wa bendi hiyo kuwapeleka kazini na kuwarudisha nyumbani miaka ya 1980.

## HABARI KIMATAIFA



Wafanyakazi wa kujitolea wakiendelea kutafuta maiti zilizokwama kwenye vifusi vya nyumba baada ya kutokea mafuriko katika mji wa Derna, nchini Libya wiki iliyopita. **PICHA: REUTERS**

# Waliofariki mafuriko Libya waongezeka

**TRIPOL,** LIBYA

WAFANYAKAZI wa vikosi vya dharura vinaendelea na zoezi la kuwatafuta maelfu ya watu ambao bado hawajapatikana kutokana na mafuriko makubwa yaliyoukumba mji wa Bandari wa Derna nchini Libya.

Wakati juhudi hizo zikiendelea, Shirika la Hilali Nyekundu la Libya limesema idadi ya vifo katika mji huo imeongezeka na kufikia watu 11,300.

Katibu mkuu wa shirika hilo Marie el-Drese, alilieleza shirika la habari la The Associated Press (AP), kwa njia ya simu kwamba watu 10,000 hawajulikani walipo katika mji huo.

Wakati huo huo waziri wa afya wa serikali ya Mashariki ya Libya, Othman Abduljaleel, alisema wameanza zoezi la kuzika miili ya watu iliyopatikana katika mji wa Derna.

Aliongeza kuwa miili mingi imezikwa kwenye makaburi ya pamoja nje ya mjio huo wakati mingine ikipelekwa katika miji na majiji ya karibu.

Ofisi ya uratibu wa masuala ya Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa OCHA, ilisema maelfu ya watu wanahitaji msaada wa dharura kufuatia mkasa huo na kutoa wito wa kupatikana dola milioni 71.4 ili kuwasaidia waathirika.

Shirika hilo lilisema kuwa karibu watu 900,000 kati ya majimbo matano wanaishi katika maeneo ambayo yameathirika moja kwa moja na kimbunga na mafuriko nchini humo.

Kimbunga kikali kilichopewa jina la Daniel kiliipiga Libya siku ya Jumapili na kusababisha mafuriko mashariki mwa Libya lakini mji uliotikiswa zaidi ni wa Derna.

Hata hivyo, miili ya maelfu ya watu waliofariki katika mafuriko hayo ambayo imekwama kwenye vifusi na baharini imezusha hofu kwa wananchi kuwa inaweza kusababisha milupuko ya magonjwa.

Bado kuna mamia ya miili chini ya majengo yaliyoporomoka na mingine imepelekwa ndani ya bahari hadi umbali wa maili 60 kutoka ufukweni.

Hofu inayotokana na dhana kwamba maiti zitasababisha magonjwa ya milipuko haijathibitishwa

Pierre Guyomarch, ambaye ni mkuu wa kitengo cha uchunguzi wa mahakama cha Msalaba Mwekundu alipinga dhana hiyo na kueleza jambo hilo halijathibitika.

"Miili ya watu ambao wamekufa kufuatia majeraha katika janga la asili au vita karibuni, kamwe haileti hatari ya kiafya kwa jamii," alisema.

Aliongeza kwamba watu walionusurika katika majanga ya asili wana uwezo wa kueneza magonjwa kuliko maiti.

**BBC**

# Marais China, Zambia wajadili uhusiano

**BEIJING,** CHINA

RAIS wa China Xi Jinping, amekutana na kiongozi wa Zambia Hakainde Hichilema mjini Beijing, wakati taifa hilo la Afrika likilemewa na madeni.

Taarifa iliyotolewa na shirika la habari la serikali ya China CCTV, ilisema Rais Xi alisema urafiki wa China na Zambia umestahamili kukabiliana na dhoruba na mabadiliko ya kimataifa.

Kiongozi huyo wa China alieleza kuwa, taifa hilo linalenga kuugeuza urafiki huo kuwa, ushirikiano wa mafanikio kati ya nchi hizo mbili kuelekea enzi mpya.

China ina hisa kubwa katika sekta ya madini nchini Zambia.

Taifa hilo lenye uchumi wenye nguvu duniani limezindua miradi ya miundombinu ikiwa ni pamoja na viwanja vya ndege, barabara na miradi ya nishati kabla ya Hichilema kuingia madarakani mwaka 2021.

Hata hivyo, Hichilema alionekana kuwa na uhusiano wa karibu na Marekani huku Rais Joe Biden, akimsifu kwa kujitolea kwake katika kuimarisha demokrasia.

**DW**

# RSF yatishia kuunda serikali Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

KIONGOZI wa Kikosi cha dharula nchini Sudan (RSF), ametishia kuunda serikali yake na mji wa Khartoum kuwa makao makuu yake.

Alisema hatua hiyo itachukuliwa jeshi la nchi hiyo litaanzisha utawala wake katika mji wa mashariki wa Port Sudan. Katika ujumbe kwenye mtandao wa X (zamani ukifahamika kama Twitter), Luteni Jenerali Mohammed Hamdan Dagalo, anayejulikana pia kama Hemedti, alisema RSF ilionyesha uvumilivu kuhusiana na maamuzi ya Mkuu wa jeshi Jenerali Abdel Fattah al-Burhan, licha ya kwamba si halali.

"Hatutaruhusu mtu yeyote kuzungumza kwa niaba ya Sudan na kudai halali kwake kufanya hivyo," aliongeza kiongozi huyo,

Tishio la kiongozi huyo wa RSF lilifuatia ripoti za vyombo vya habari vya serikali kwamba serikali inayoongozwa na jeshi ina mpango wa kujenga ikulu ya rais na makao makuu ya wizara yake ya mambo ya nje katika Bandari ya Sudan kwenye jimbo la Bahari Nyekundu.

Jiji hilo limekuwa likitumika kama kituo cha uendeshaji wa serikali tangu mzozo ulipozuka kati ya jeshi la kawaida na kikosi cha RSF mjini Khartoum katikati ya mwezi Aprili.

# Russia yawatimua wanadiplomasia wawili kwenye ubalozi wa Marekani

**MOSCOW,** RUSSIA

WAFANYAKAZI wawili wa ubalozi wa Marekani nchini Russia, wamepewa siku saba wawe wameondoka kwa madai wana matendo yasiyofaa.

Wanadiplomasia hao wametajwa kuwa ni Jeffrey Sillin na David Bernstein, ambao walikuwa wakifanya kazi ndani ya ubalozi wa marekani.

Taarifa kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Russia, ilisema Sillin na Bernstein wanatakiwa kuondoka ndani ya nchi hiyo katika muda huo waliopewa.


Wizara hiyo ilisema wafanyakazi hao walifanya shughuli haramu na kuwa na mawasiliano na mfanyakazi wa zamani wa Ubalozi wa Marekani huko Vladivostok, Robert Shonov, ambaye anatuhumiwa kukusanya habari kuhusu vitendo vya wanajeshi wa Russia nchini Ukraine.

Robert Shonov alifanya kazi katika Ubalozi wa Marekani huko Vladivostok kwa zaidi ya miaka 25 hadi Russia ilipoamuru kufukuzwa kwa wafanyakazi maalum wa misheni ya Marekani mnamo 2021.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAIMUNA ABACCY MKETO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S **4827/0038** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. PETER CLAVER HIGH SCHOOL DODOMA** mwaka 2020. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DOD/DOD/2918/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NAFTAL RASHID KIHWELO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA **BAJAJI** YENYE USAJILI **MC 633CQB** AINA YA TVS RANGI YA KIJANI.YEYOTE ATAKAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI JALADA NAMBA **PHQ/IRI/IRI/853/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**WILSON NAHASON MWAMBAMBALE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI **MC939 CFC** IKIWA NA JINA LA USAJILI WA KAMPUNI YA MOHAMED ENTERPRISES LTD. YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA NAMBA **;IRI/IRI/RB/391694/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EMMANUEL EZEKIEL BIYOLERO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T952 ASJ.** Chassis No **LH1000050651** Engine No **10499502030532** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/2264/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASIA MAJIDI MRETA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COASTER** yenye usajili namba **T 121 DRJ,** CHASSIS NAMBA: **HDB510004456** na ENGINE NAMBA: **1HD0137473.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/ARU/ARU/2363/2023**

## KUPOTEA KWA VYETI



**RAHEL IBRAHIM TWEVE** anatangaza kupotea kwa cheti na result slip ya kidato cha nne vyenye index namba **S1161-0062** vilivyotolewa na baraza la mtihani la taifa kupitia **MAWELEWELE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2012 na result slip ya kidato cha sita chenye index namba **S4929-0529** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TINDE GIRLS HIGH SCHOOL** mwaka 2015. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:**KBA/PS/B.2/29/VOLXXXV/**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 454 LA 2023**

**GOLDEN PEAK TRADING LTD MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SERAFINA LTD ......................MDAIWA /WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**SERAFINA LTD**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

..........................................................................Amefungua /wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 02/10/2008 Saa 3:00AM. Asubuhi/Mchana mbele ya Mh J.W.SILLAS. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hivo bila kukosa.

..............................................

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ua Wilaya ya .KINONDONI**

**Kituo cha KINONDONI Mkoa ..............DAR ES SALAAM**

**Shauri la Madai Na ......................................................247 2023**

**Jina la mdai ..........................................DIAMOND TRUST BANK**

**Jina la Mdaiwa.......................................JACOB MUSSA MAGINA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za Kuratibu madai Katika Mahakama za Mwazo)**

**Kwa JACOB MUSSA MAGINA**

Kwa kuwa Mdai /Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)
**FIKA MAHAKAMANI KWA AAJILI YA HUKUMU**
Kwa
Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii terehe 20 Mwezi 09 Mwaka 2023 saa 4:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi /mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 09 Mwaka 2023.

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KINONDONI
WILAYA YA KINONDONI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya KINONDONI**
**Kituo cha KINONDONI**

**Shauri la Madai Ndoa Na 177...../2023**

**Jina la mdai......................................................DIAMOND TRUST**

**Jina la Mdaiwa....................................................ANETH JERRY**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa ANETH JERRY**
**0758 168262**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (eleza hapa habari za madia)
Wnatakiwa kufika katika mahakama ya mwanzo KINONDONI bila kukosa siku hiyo. Madai ya fedha 28,484673.
Hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 25 Mwezi 09 Mwaka 2023 saa 08:30 asubuhi /mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea
ANGALIZO kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 11 mwezi 09 mwaka 2023

HAKIMU

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HEPPY BENEDICT ALEX** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI (BOXER) YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 951** ATP KWA YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. **MOR/KIL/RB/1906895/2023**

## MAREKEBISHO YA MNADA WA HADHARA

Kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana za wadaiwa sugu. Mnada utaendeshwa na madalali tajwa hapo chini kwa idhini ya **Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd** kama ilivyotangazwa gazetini:-

| Mdhamini/ Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada/ Dalali |
|---|---|---|
| Bernard Daud Nkeyemba | Nyumba-Kinzudi Madale DSM | 11. 09.2023 (**Marudio**) DENNESTO CO. LTD |
| Gregory Isdory Wenceslaus | Plot – Kimara-King'ong'o -DSM **Plot- Kibamba Mkuranga** | 15.09.2023 (**Marudio**) White miracles **12.09.2023** |
| Yahaya Khalid Ally | Nyumba- Kihonda Morogoro | 22.09.2023 (**Marudio**) Diamond Credit |
| Bakari Fakhi bakari | Nyumba- iliyopo Kinyamwezi-DSM | SEPCO Debt Collector 06.10.2023 |
| Hamida Mohamed Aley | Plot- Tandika (Mtaa Nyambwera) | RAPITECH Solutions Ltd – 26.09.2023 |
| Jerome Jerome Tesha | Plot – Mkuranga (Utungemwago) | RAPITECH Solutions Ltd – 28.09.2023 |
| Biswaro Zebedayo Msase | Nyumba (Kwembe) Mloganzila-DSM | RAISSA CO. LTD 29.09.2023 (**Marudio**) |
| Ridhiwan Khutuba Kyela/ Jonathan Shirima | Nyumba- ipo Kibondemaji Mbagala | GEMSUD Investment Ltd – 27.09.2023 |
| Hilda Archady Kikatuka | Nyumba - Mbugani Kishiri Mwanza | Mase International Ltd 21.09.2023 |
| Elizabeth Maxmillian Komba | Home chattels | GEMSUD Investment Ltd - 20.09.2023 |

**Masharti Mengine:**
Minada yote itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga: MASE – 0784717164/0743885084**
**SEPCO- 0715683777; White Miracles-0782359900**
**DENNESTO-0658896226; Diamond; 0789455445**
**GEMSUD-0652113262; RAPITECH-0628866132**




***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 00745 700 710.***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MBWA mmoja wa jirani wa maeneo ya Kinondoni Msisiri, alionekana kuvutiwa na kiroba kilichotupwa upenuni mwa nyumbani moja. Ni moja kati ya viroba ambavyo hutupwa usiku au alfajiri na vijana wanaokusanya taka kwenye nyumba za watu na kupewa ujira kidogo. Wao badala ya kwenda kutafuta maeneo ya kutupa, hupita vichochoroni na kama hajaonekana anautupa mzigo na kuendelea na safari yake. Ilitokea kwenye nyumba moja huko, na mbwa huyo alipouvuta, viungo vya mwili wa binadamu vilianguka. Majirani wa kwanza kuona walipiga kelele na watu wakajazana. Akinamama waliangua vilio. Viungo vilihifadhiwa kwa kufunikwa. Polisi walianza msako. Kwa kuanzia tu, wakaanza kuwakamata wazoa taka na waokota chupa za kwenda kuuza, wote wa maeneo hayo na jirani wanaofahamika tayari kwa mahojiano na uchunguzi, wakihisiwa kuwa huenda mmoja wao au zaidi kuhusika na mauaji. Ni maiti ya nani? Na muuaji ni nani? Fuatilia mwanzo hadi mwisho kujua mkasa mzima ulivyokuwa.

## MAITI KWENYE KIROBA-26

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

Pamoja na kuwa ni mpelelezi wa kiwango cha juu Afrika, lakini pia alikuwa mtaalam kwenye masuala ya kijamii hasa mambo yanayohusu mahusiano na mapenzi.

Moja ya kitu ambacho alichokuwa na uzoefu nacho ni kwamba ni vigumu sana kumshawishi mwanamke kwa njia yoyote ile kama hakupi nafasi ya kukusikiliza.

Mwanamke akikataa kumpa nafasi mwanaume basi hawezi kufanya chochote kile. Lakini kama atatoa nafasi, basi kwa wanaume kwenye sanaa ya kushawishi anakuwa amekwisha.

Eddy ni mmoja wa wanaume ambao wana uwezo mkubwa wa kuongea na kushawishi.

Kitendo cha kumsikiliza na kuanza kuagiza chakula, alikuwa ameshamaliza kila kitu.

“Na mimi niletee ndizi mbili za kuchoma, mishikaki minne na juisi ya embe kama ipo.” Eddy naye aliagiza.

Eddy alichokuwa akihitaji ni kupata siri nyingi za Charton aliyemuua mkewe Tessy. Kwa sababu walikuwa wameachana kama alivyodai Nancy na kuonekana kulalama kuachwa na kuchukuliwa Rukia alijua atazipata tu.


Hata hivyo moja kati ya vitu anavyotakiwa kuvifanya ili azipate kwa urahisi zaidi si kwa kujifanya polisi au mpelelezi. Urafiki pekee ndiyo utamfanya kuua tembo kwa ubua. Ni kutengeneza urafiki wa kimapenzi japo wa muda. Alijua hiki ni kipindi ambacho Nancy ana maumivu ya kuachwa na Charton, hivyo ingekuwa rahisi kumshawishi.

Ilipita dakika tano hivi Eddy hakuongea lolote, badala yake walikuwa akimhimiza Nancy ale na kumuweka sawa kisaikolojia.

Kubembelezwa na kusifiwa uzuri kulimfanya Nancy kusahau kila kitu kwa muda. Kumsahau Charton na rafiki yake Chimozi pia.

Alijiona kama kuna nyota mpya ya jaha inamjia. Aliona kama yote yanayotokea ni bahati ya mtende iliyomjia kwa kudra za Mwenyezi Mungu.

Kuachana na Charton, halafu kwa namna ambayo haikutarajiwa kukutana na rafiki wa rafiki wa aliyekuwa mpenzi wake. Yaani aliyekuwa mpenzi wake ana rafiki aitwaye Chimozi, lakini naye pia ana rafiki yake ndiye huyu ambaye anaonekana kama ana lake jambo.




**“Sasa kama tulivyoahidiana, Jumamosi ijayo nitafika hapa hapa kukuchukua sawa?”**

Kwa Eddy, asilimia kubwa ilikuwa ni kazi tu, lakini kila akimwangalia Nancy ni moja kati ya wanawake walioumbwa wakaumbika.

Alikuwa na sifa zote za kuitwa mwanamke mzuri na mrembo. Tatizo ni kwamba amejiachia na kuanza kunenepa.

“Mbona huli mrembo?”

“Nakula.” Akajibu kwa aibu kidogo.

Dakika kumi ambazo Eddy aliongea na Nancy zilimfanya mwanadada huyo kujiona yuko sehemu salama.

Alikutana na mtu mchangamfu, mcheshi na mwenye nidhamu, adabu na heshima.

Siyo wale ambao siku ya kwanza tu akikutana na mwanamke anamfanya kama ameshamuoa miaka mitatu iliyopita.

“Kwani wewe unaishi wapi?” Nancy akauliza.

“Victoria.” Akajibu.

“Nimefurahi sana kukutana na wewe.”

“Na mimi pia.”

“Lakini nasikia wewe una uhusiano na Charton?” Eddy akauliza kiujanja.

“Unajua mimi nimetokea kukuheshimu. Kwa muda mfupi tu nimekupa muda wangu huu kuwa na mimi, kwa hiyo utumie vizuri, siyo kunitajia mtu huyo. Unaweza kunifanya nikaondoka hapa.”

“Samahani sana mrembo. Ila niliambiwa tu na Chimozi kuwa mna uhusiano, kama aliniongopea basi, naomba unisamehe, tuendelee na mambo yetu.”

“Hapa nimekuja kufurahi, siyo kuomboleza kisa cha mtu huyo ambaye kwa sasa sipendi hata kumsikia. Leo tusiongee chochote, ni siku ya furaha, ila kama tutaendelea kuwa wote kama tunavyoahidiana, basi nitakwambia mambo mazito yaliyonipata kuhusu mtu huyo, na yale ambayo ameyafanya.”

Eddy alijiona mshindi tayari, kwani kile alichokitaka mpaka kumtaka Nancy kimapenzi tayari kimeshatimia.

Kutaka undani na ushahidi kuhusu Charton. Amemuua mkewe kwa sababu za kimapenzi, lakini nini kilitokea? Nini kilikuwa nyuma yake. Ilianzaje mpaka ikawa hivyo? Ndicho kilichobaki kabla ya kumtia mbaroni.

Baada ya kukubaliana kuwa wapenzi, Eddy alimtahadharisha Nancy, ingawa kwa utani alikuwa akiimaanisha.

“Nadhani hakuna tena haja ya kumwambia Chimozi kitu chochote mimi na wewe, labda mwenyewe akuulize sawa?”

“Kwa nini?” Akauliza Nancy akiwa anacheka.

“Ataanza kukudodosa vitu vingi, ilikuwaje hapo, mliondoka saa ngapi, mliondoka wote, ilikuwaje, yaani ili mradi tu, tena kwa sababu yeye hakuwepo, atakuwa na wasiwasi na mimi.”

“Wala. Kwanza hata simpigii mpaka yeye mwenyewe anipigie. Na hata akinipigia simwelezi kitu chochote. Tena nimekumbuka, akiuliza habari zako nitamwambia kuwa hukuja kama yeye ambavyo hakufika.”

Alijipigia makofi kimoyomoyo kwa sababu alichokitaka kimekuwa.

Hakutaka Nancy ampigie simu Chimozi kwa sababu atamwambia tu kuwa mtu huyo simjui na hajawahi kuwa na mawasiliano na mtu kama huyo hivyo ataanza kuwa na wasiwasi.

Kilichotokea ni kwamba Eddy amempata Nancy kwa bahati nasibu sana. Namba alizopewa na Mboneka. Alipompigia Nancy mwenyewe ndiye aliyejichanganya na kuuliza anayepiga ni Chimozi au Sunguruma. Eddy akaunganisha kuwa yeye ni Chimozi. Akamwambia wakutane pale. Lakini aliyewasili hapo hakuwa Chimozi. Akamuongopea kuwa Chimozi, amepata na matatizo njiani hatokuja tena na yeye ni rafiki yake ambaye waliahidiana kukutana hapo ingawa ana taarifa ya mwanadada mmoja kuwepo hapo.

Walitoka na kutembea kwa miguu. Nancy alidhani wanakwenda kupanda basi. Walipofika maeneo ya Mwenge sokoni ndipo aligundua kuwa jamaa ana gari.

“Enhee unaishi wapi nikupeleke bibie.”

“Boko.”

Gari ilitafuna lami mpaka Boko.

“Nashukuru nishushe hapa hapa nimefika.”

“Sasa kama tulivyoahidiana, Jumamosi ijayo nitafika hapa hapa kukuchukua sawa?”

“Saa ngapi?”

“Saa mbili usiku. Tunaweza kuupitisha usiku mmoja na wewe? Yaani usirudi nyumbani?”

“Sawa wewe tu.”

Nancy alijiona ni mwanamke mwenye bahati zake.

“Mwanamke niliyeombewa dua na wazazi wangu. Niliyetolewa mikosi. Niliyeoga maji ya bahari. Katoka bwana wa maana, kaingia bwana wa sheria yake.” Akajitapa kimoyomoyo.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# CDF ANAVYOWEKA MAZINGIRA MAZURI MASHUJAA KUFIKIA MALENGO LIGI KUU

**Na Mwandishi Wetu**

KUFUATIA kuwepo kwa mazingira mazuri yaliyowekwa na Mkuu wa Majeshi, Jenarali Jacob Mkunda, katika kuendeleza michezo na kufikia malengo ya kupeleka timu yake kwenye michuano ya kimataifa, uongozi wa klabu ya Mashujaa FC ya Kigoma umejipanga na kudhamiria kufikia malengo hayo.

Katika kuhakikisha wanafikia malengo ya kumaliza ligi wakiwa miongoni mwa klabu za 'Top Four', benchi la ufundi la timu hiyo limedhamiria kufanya vizuri kwenye michezo yake yote na wataendelea kusaka pointi tatu kwenye mchezo unaokuja wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Meja IY Mgaya, alisema Mkuu wa Majeshi ameweka mazingira mazuri ambayo yanatoa nafasi kwa timu kupambana na kufikia malengo yao.

Alisema Mashujaa FC imekuwa ikiishi kwenye mazingira mazuri tangu kupanda kwenye ligi na inasafiri kwa wakati kufika kwenye mkoa kucheza michezo yao ya Ligi Kuu.

"Tunataka kuhakikisha tunapata nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa kwa kumaliza katika nafasi nne za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu kutokana na mazingira mazuri ambayo afande CDF ameyaweka kwa timu zetu," alisema Meja Mgaya.

Aidha, alisema uwepo wa mashabiki wenye 'Mzuka' mkoani Kigoma anaamini uwanja wao wa Mashujaa mkoani humo utakuwa machinjio ya timu pinzani.

"Tuna mchezo dhidi ya Ihefu leo (jana), naamini hata kwenye michezo ijayo tutafanya vizuri na kuondoka na pointi zote tatu muhimu na kuendelea kuwa kwenye nafasi nzuri," alisema Meja Mgaya.

Kuelekea kwenye michezo ijayo ya ligi kuu, Kocha wa timu hiyo, Mohamed Abdallah 'Bares', amesema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye kila mchezo.

"Tunafahamu ligi ni ngumu kwa sababu kila timu imejiandaa, kama Mashujaa tumejiandaa vizuri na kila mechi kwetu itakuwa kama fainali kuainzia ile tutakayocheza nyumbani na hata ugenini, tumejipanga na tunaendelea kujiimarisha, " alisema Bares.

Kocha huyo ameweka wazi namna wachezaji wake walivyojiandaa na kuwa na shauku ya kufanya vizuri kwenye ligi msimu huu wa kwanza.

"Kila mchezaji ana hamasa ya kufanya vizuri, yaani kila mchezaji mbele yetu wanakuwa na hamasa nao, kwangu hili ni jambo jema na la muhimu kuona ambavyo wachezaji wetu wanapambana na kuwa na utayari muda wote, tunaamini tutafanya vizuri kwenye michezo yetu," alisema Bares.


Timu hiyo iliyopanda Ligi Kuu kwa kishindo msimu huu, inamilikiwa na Jeshi la Wananchi (JWTZ) chini ya uratibu wa karibu na Kurugenzi ya Michezo na Utimamu wa Mwili, inayoongozwa na Martin Msumari.

Kwa muda mrefu sasa Jeshi la Wananchi limekuwa na mchango mkubwa kwenye kukuza soka hapa nchini ambapo wamekuwa wakiwapa nafasi vijana wenye vipaji kujiunga na timu zao.

Aidha, wamekuwa wakisaidia kukuza soka la vijana na kuwa mdau mkubwa wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Mashujaa FC ilipanda daraja msimu huu baada ya kufanikiwa kuibuka na ushindi wa jumla kwenye mchezo wa 'Play Off' dhidi ya Mbeya City kwa ujumla ya ushindi wa mabao 4-1.

Mpaka sasa Mashujaa FC imecheza michezo miwili (kabla ya mchezo wa jana) na imeshinda mchezo mmoja dhidi ya Kagera Sugar (1-0) na kutoka sare mmoja dhidi ya Geita Gold.




Mkaguzi wa Huduma ya Tigo, Mayagi Nyega (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi, mshindi wa shindano la ' Tigo Cha Wote', Abasi Mwinyi, katika hafla iliyofanyika Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Transit Camp ilivyopania kurejea Ligi Kuu 2024/25

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa klabu ya Transit Camp, inayoshiriki Championship umesema kutokana na sapoti wanayoipata kutoka kwa Mkuu wa Majeshi, Jenarali Jacob Mkunda, wamepania kupanda daraja na kucheza Ligi Kuu msimu ujao.

Transit Camp tayari imecheza mchezo mmoja kwenye ligi yao dhidi ya KenGold ambapo wamefanikiwa kuvuna alama moja.

Akizungumza na gazeti hili, Mwenyekiti wa klabu hiyo, Meja SD Tandika, alisema lengo lao msimu huu ni kuhakikisha timu hiyo inapanda daraja na msimu ujao kucheza Ligi Kuu.

"Tumejipanga na tunaendelea kufanya hivyo, tumeanza vizuri kwenye mchezo wetu wa ligi, kama timu ni kuhakikisha tunapanda Ligi Kuu, na tunaweza kufikia malengo haya kwa sababu tumedhamiria kufanya hivyo msimu huu," alisema Meja Tandika.

Kuelekea mchezo wao ujao dhidi ya Mbeya City, Kocha wa timu hiyo Saidi, alisema kila mchezo kwao wanauchukulia kama fainali kwa kuwa malengo yao ni kufanya vizuri msimu huu.

"Tutacheza na Mbeya City mwishoni kwa wiki hii, malengo yetu ni pointi tatu, tunaiheshimu Mbeya City kwa uzoefu wao, lakini kwetu kila mchezo ni kama fainali kutokana na malengo yetu msimu huu," alisema Saidi.

Alisema mechi moja waliyocheza imewapa mzuka wa kutaka kuendelea kufanya vizuri zaidi kwa kuwa hawajapoteza pointi zote tatu na wamefanikiwa kuvuna pointi moja.

Kwa mujibu wa taratibu, timu zote teule za Jeshi zipo chini ya Kurugenzi ya Michezo na Utimamu wa Mwili wa Jeshi hilo inayoongozwa na Kanali Martin Sumari

Msemaji wa klabu hiyo, Willy Kulwa, alisema Transit Camp FC imedhamiria kufanya vizuri kwenye ligi Championship kutokana na namna uongozi wa Jeshi unavyoisimamia timu hiyo

Alisema licha ushindi walioupata Mbeya City kwenye mchezo wao uliopita dhidi ya Green Warriors, hauwafanyi Transit Camp kuwaogopa wapinzani wao hao watakaokutana na jumamosi ijayo.

## Gadiel kutibua kiungo Future FC

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate FC, Ernest Middendorp , amewapa majukumu nyota wake wawili, Michael Gadiel na Aziz Andambwile kuhakikisha wanawazuia viungo hatari wa Future FC katika mchezo wa hatua ya pili ya Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa kesho jijini Dar es Salaam.

Gadiel, beki wa kushoto amebadilishiwa majukumu hayo kushirikiana na Andambwile kusaidia katika nafasi ya kiungo mkabaji ili kuwazuia viungo wa Future FC inayoongozwa na Ahmed Refaat.

Singida Fountain Gate FC wanaendelea na mazoezi yao uwanja wa Azam Complex, uliopo Chamazi kwa ajili ya mchezo huo wa mkondo wa kwanza kuwania kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana mara baada ya mazoezi hayo, Mkurugenzi wa Ufundi wa timu hiyo, Ramadhani Nsanzwirimo, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na hawana majeraha huku wachezaji wote wako tayari kwa mchezo huo.

Alisema benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Middendorp wanafanyia kazi ubora wa wapinzani wao hasa imara wao katika safu ya kiungo ambapo mechi zilizopita walifanya mashambulizi kutokea kati.

"Mpira wa miguu ni mbinu, tumeanza kufanyia kazi ubora wao lakini kuandaa wachezaji wetu, Kocha wetu amewapa majukumu maalum Gadiel na Andambwile kuhakikisha wanawakabili vyema viungo wa wapinzani wetu kwa kusaidiana na safu yetu ya viungo, lakini pia tunapaswa kumudu presha ya mashabiki wetu ili tucheze kwa malengo," alisema Mkurugenzi huyo.

Aliongeza kuwa Future FC ni timu nzuri, wana wachezaji wazuri na wameweza kusumbua vigogo wa ligi ya Misri hali ambayo itawafanya wao (Singida FG) kucheza kwa tahadhari kubwa ili kuweza kupata ushindi kwenye mechi hiyo ya nyumbani.

## Washindi wa tigo wapewa zawadi zao

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya washindi 26,000 kutoka maeneo mbalimbali nchini wamejishindia zawadi kila mmoja kutoka kampuni ya huduma za simu ya Tigo baada ya kushiriki shindano la 'Tigo cha Wote'.

Washindi hao kila mmoja amekabidhiwa pesa Shilingi milioni moja baada ya kuibuka washindi kwenye shindano hilo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi hao jijini Dar es Salaam, Meneja wa wateja maalum wa kampuni hiyo Mary Rutta, alisema washindi hao walishiriki kwa nyakati tofauti shindano hilo litakalodumu kwa siku 90.

"Leo tunayo furaha kubwa kuwa na baadhi ya washindi wa shindano hili, ambao hawa ni washindi wa sh. milioni moja kila mmoja, lakini niwakumbushe Watanzania kwamba kila siku tunatoa zawadi ikiwemo hizi pesa taslimu," alisema Rutta.

Mmoja wa washindi wa shindano hilo, Marry Kavishe, alisema kuwa fedha hizo zitamsaidia kununua mashine ya cherehani ili kuhakikisha anakuza biashara yake kwa kuongeza kipato.

"Ninatarajia kutumia fedha hizi kwa ajili ya kununua cherehani mpya ambayo itanisaidia kukuza biashara yangu na kujiongezea kipato," alisema.

Naye mshindi mwingine, Kenedy Shao, alisema amefurahia kuibuka kidedea katika kampeni hiyo na fedha alizopata zitamsaidia kulipia ada ya shule kwa mtoto wake.

"Nimefurahia kupata nafasi ya kushinda katika shindano hili, ninatarajia kutumia fedha hizi kumlipia ada mwanangu kwani zimekuja wakati mwafaka," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### JAMES KUMRITHI CARVAJAL

BEKI wa Chelsea na England, Reece James mwenye umri wa miaka 23 ameteuliwa na Real Madrid kama mbadala wa muda mrefu wa Mhispania Dani Carvajal, 31. James alisaini mkataba wa miaka sita na The Blues mnamo 2022. (***Diario AS***)

### BARCO AWANIWA CITY

KLABU ya Manchester City imekubali mkataba kimsingi wa kumsajili kinda wa Boca Juniors, Valentin Barco mwenye umri wa miaka 19 ambaye anacheza nafasi ya beki wa kushoto. (***Mjerumani Garcia Grova on X***)

### ODEGAARD KUONGEZA

KIUNGO wa kati wa Arsenal na Norway, Martin Odegaard mwenye umri wa miaka 24 na mlinzi wa England, Ben White mwenye miaka 25 wanatazamiwa kuweka mustakabali wao wa muda mrefu kwa washikabunduki kwa kusaini mikataba mipya. (***football.london***)

### MEJBRI ASAKWA

MCHEZAJI wa Manchester United, Hannibal Mejbri mwenye umri wa miaka 20 anasakwa na Besiktas 20. (***Sun***)

### SANCHO AJIANGALIE

WINGA wa Manchester United na England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, anahitaji kujiangalia kama anataka kuokoa maisha yake ya soka akiwa na Mashetani Wekundu baada ya kutofautiana na kocha wake Erik ten Hag, amesema kiungo wa zamani wa United, Gordon Strachan. (***Mirror***)

### LINGARD AWANIWA

KIUNGO wa a zamani wa England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 30, anaendelea kufanya mazoezi na West Ham, lakini amepokea ofa kutoka Uturuki, Saudi Arabia, Qatar na MLS tangu aondoke Nottingham Forest. (90 Min)

### PALHINHA KUTUA BAYERN

KIUNGO wa kati wa Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28 bado anaweza kuhamia Bayern Munich licha ya kusaini mkataba wa nyongeza na Fulham. (***Bild***)

### ALCANTARA HASITISHIWI

LIVERPOOL hawana nia ya kukatiza mkataba wa Thiago Alcantara ili kumuwezesha kiungo huyo wa kati wa Hispania mwenye umri wa miaka 32 kupata uhamisho wa kutua Uturuki. (***Football Insider***)

### DENNIS AWANIWA UTURUKI

KLABU ya Istanbul Basaksehir imekubali mkataba wa mkopo kumsaini mshambuliaji wa Nigeria, Emmanuel Dennis mwenye umri wa miaka 25 kutoka Nottingham Forest. (***Fabrizio Romano***)

### TERRY ATAKIWA SAUDIA

KLABU ya Al-Shabab ya Saudi Arabia imeanza mazungumzo na beki wa zamani wa Chelsea na England, John Terry kuhusu nafasi ya ukocha. (***Nicolo Schira***)

### BALOTELLI ATAKIWA




ADANA Demirspor yuko kwenye mazungumzo ya kumsajili tena mshambuliaji wa zamani wa Italia, Mario Balotelli mwenye umri wa miaka 33 kutoka klabu ya Uswisi ya Sion. (***Ajansspor- In Turkish***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA









# MESSI, HAALAND, MBAPPE WAWANIA TUZO YA FIFA

**NYON,** Uswisi

●●● Mchuano mkali katika tuzo hizo unatarajiwa kuwa kati ya Messi na...

LIONEL Messi, Erling Haaland na Kylian Mbappe wanaongoza orodha ya wachezaji 12 wanaowania tuzo ya mchezaji bora wa kiume wa Shirikisho la soka la kimataifa, FIFA, huku kiungo wa kati wa England, Declan Rice pia akiteuliwa baada ya nahodha wa klabu ya zamani ya West Ham United kubeba kombe la Europa Conference.

**Nahodha wa Argentina Messi, ambaye sasa anachezea klabu ya MLS Inter Miami analenga kushinda tuzo hiyo kwa mara ya tatu baada ya kupewa heshima hiyo mwaka wa 2019 na 2022.**

Lakini licha ya kuisaidia Argentina kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia huko Qatar 2022, Messi anakabiliwa na ushindani mkali kutoka kwa fowadi wa Manchester City Haaland baada ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway kufunga mabao 52 huku kikosi cha Pep Guardiola kikibeba mataji matatu, Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na FA msimu uliopita.

Julian Alvarez, Marcelo Brozovic, Kevin De Bruyne, Ilkay Gundogan, Rodri, Khvicha Kvaratskhelia, Victor Osimhen na Bernardo Silva pia wameingia kwenye orodha hiyo.

Hispania ambayo ilishinda Kombe la Dunia la Wanawake kwa mara ya kwanza nchini Australia mwezi uliopita, ina wachezaji wanne kwenye orodha ya wachezaji 12 walioteuliwa kuwania tuzo ya wanawake huku Aitana Bonmati, Jenni Hermoso, Mapi Leon na Salma Paralluelo wote wakiwa kwenye mbio za kuwania ufamle huo.

Linda Caicedo, Rachel Daly, Kadidiatou Diani, Caitlin Foord, Mary Fowler, Alex Greenwood, Amanda Ilestedt, Lauren James, Sam Kerr, Hinata Miyazawa na Keira Walsh pia wameteuliwa, huku Lindsey Horan ndiye mchezaji pekee wa Marekani aliyeingia kwenye orodha hiyo.

Upigaji kura kwa ajili ya tuzo za nane za kila mwaka ulifunguliwa Alhamisi kwenye mtandao wa FIFA.com na utafungwa katikati ya Oktoba.

Makocha wa timu za taifa, manahodha, waandishi wa habari na mashabiki ndio wanaounda orodha ya wapiga kura.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,152,9

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
BRIGHTON
1 | 2.26
X | 3.90
2 | 2.85

tigo pesa SportPesa
WASHINDI WA MAOKOTO Deilee!
1. Abraham Kibona - 0657 694 XXX
2. Stephen Berinadi - 0672 641 XXX
3. Mkesha Saad - 0673 466 XXX
4. Fredrick Simkoko - 0679 907 XXX
5. Paulo Paulo - 0712 677 XXX
6. Said Hussein - 0712 827 XXX
7. Gift Kangale - 0712 996 XXX
8. Kulwa Chamba - 0716 383 XXX
9. Yusuph Mdoe - 0716 808 XXX
10. Msafiri Msafiri - 0716 980 XXX
20,000/= KWA KILA MMOJA

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# JADON SANCHO ATEMWA KIKOSI CHA KWANZA MAN UNITED

**MANCHESTER,** England

JADON Sancho atafanya mazoezi nje ya kikosi cha kwanza cha Manchester United kufuatia mzozo wake na kocha Erik ten Hag.

Ten Hag alimwacha Sancho kwenye kichapo cha 3-1 kutoka kwa Arsenal kabla ya mapumziko ya kimataifa, na akasema kukosekana kwa winga huyo kulitokana na kutofanya vizuri kwenye mazoezi.

Maoni hayo yalimfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kudai kwenye mitandao ya kijamii kwamba alifanywa "mbuzi wa kafara" na kupendekeza kwamba maneno ya kocha huyo raia wa Uholanzi hayakuwa ya kweli.

Taarifa kutoka kwa Mashetani Wekundu ilisema wataangalia kutatua kile wanachoita "suala la nidhamu ya kikosi", wakati ambapo Sancho atasalia kwenye "mpango wa mazoezi binafsi".

Baada ya kushindwa kwenye Uwanja wa Emirates mnamo Septemba 3, Ten Hag alisema:

"Jadon kwa uchezaji wake mazoezini hatukumchagua.

Lazima ufikie kiwango kila siku Manchester United na tunaweza kufanya maamuzi katika mstari wa mbele. Kwa hiyo kwa mchezo huu hakuchaguliwa."

Sancho alijibu kwa kusema: "Tafadhali usiamini kila kitu unachosoma.

Sitaruhusu watu kusema mambo ambayo si ya kweli kabisa, nimejiendesha vizuri sana kwenye mazoezi wiki hii.

Naamini kuna sababu nyingine za jambo hili ambazo sitaingia nazo, nimekuwa mbuzi wa kafara kwa muda mrefu jambo ambalo si sawa!"

Mustakabali wa Sancho pale Old Trafford sasa unaonekana kuwa mashakani baada ya kipindi kigumu tangu kuhama kwake kwa pauni milioni 73 kutoka Borussia Dortmund msimu wa joto wa 2021.

Amefunga mabao 12 pekee katika mechi 82 akiwa na Mashetani Wekundu na alihusishwa na kuhamia Saudi Arabia kabla ya tarehe ya mwisho ya wiki ya usajili, wiki iliyopita.

# *Walker ajifunga Man City hadi 2026*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imethibitisha kuwa beki mkongwe, Kyle Walker amesaini mkataba mpya hadi mwaka 2026.

Walker alikuwa mlinzi muhimu wakati katika kampeni ya Man City ikishinda mataji matatu msimu wa 2022/23.

Pia amepambana na ushindani kutoka kwa Reece James na Trent Alexander-Arnold katika miaka ya hivi karibuni kwa nafasi ya beki wa kulia wa kikosi cha kwanza cha England.

Walker aliiambia tovuti ya klabu, "Hatuna visingizio. Kila kitu tulichonacho hapa, vifaa, wapishi, wapiganaji, wataalamu wa lishe,vyote ni vya hali ya juu.

Kwa hiyo ikiwa wanatoa kile wanachoweza kufanya au kwa ubora wao haitupaswi kuwa na kisingizio cha kutotoka nje. Hakuna visingizio".

"Na tunapaswa kudai hilo kutoka kwetu kama kikundi cha wachezaji. Tunajua kwamba klabu hii na shirika hili wameleta ubora zaidi katika kile wanachofanya.

Kwa hiyo tunahitaji tu kuhakikisha kuwa tunajitokeza kila siku ya mchezo, kuweka alama tatu kwenye ubao na kuendelea na inayofuata."

Hapo awali Walker alikuwa amethibitisha kuwa anakaribia kusaini mkataba mpya hapo Etihad mapema Septemba, pia akikiri kuwaniwa na Bayern Munich.

Baada ya kutoka Tottenham, Walker mwenye umri wa miaka 33 alijiunga na City mwaka wa mwaka 2017 kwa kitita cha pauni milioni 45 na kupanda hadi pauni milioni 50.



## HABARI MICHEZO


911,993/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.16/09/23 | 17:00 | Bristol City vs West Bromwich Albion | 2.41 | 3.25 | 2.80 |
| 02.16/09/23 | 17:00 | Kilmarnock FC vs Hibernian FC | 2.48 | 3.30 | 2.70 |
| 03. 16/09/23 | 17:30 | Rio Ave FC vs FC Famalicao | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 04. 16/09/23 | 19:00 | Inter Milano vs AC Milan | 2.16 | 3.35 | 3.15 |
| 05. 16/09/23 | 19:30 | VfL Bochum vs Eintracht Frankfurt | 2.80 | 3.50 | 2.27 |
| 06. 16/09/23 | 20:00 | USL Dunkerque vs Grenoble Foot | 2.65 | 3.10 | 2.60 |
| 07. 16/09/23 | 20:00 | Rodez Aveyron Football vs Angers SCO | 2.70 | 3.15 | 2.55 |
| 08. 16/09/23 | 20:00 | Paris FC vs Amiens SC | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 09. 16/09/23 | 20:30 | SK Sturm Graz vs FC Salzburg | 2.70 | 3.30 | 2.24 |
| 10. 16/09/23 | 21:45 | Cardiff City vs Swansea City | 2.55 | 3.25 | 2.65 |
| 11. 17/09/23 | 13:30 | Cagliari Calcio vs Udinese Calcio | 2.85 | 3.25 | 2.39 |
| 12. 17/09/23 | 15:00 | Getafe CF vs CA Osasuna | 2.50 | 2.90 | 2.95 |
| 13. 17/09/23 | 15:30 | FC Twente Enschede vs Ajax Amsterdam | 2.65 | 3.35 | 2.48 |
| 14. 17/09/23 | 16:00 | Frosinone Calcio vs Sassuolo Calcio | 2.75 | 3.35 | 2.40 |
| 15. 17/09/23 | 16:30 | FC Heidenheim vs Werder Bremen | 2.27 | 3.70 | 2.70 |
| 16. 17/09/23 | 17:15 | US Catanzaro vs Parma Calcio | 2.42 | 3.00 | 2.65 |
| 17. 17/09/23 | 19:00 | ACF Fiorentina vs Atalanta BC | 2.35 | 3.45 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 16/09/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3813 | CSKA Moscow vs Kryliya Sovetov | 1.70 | 3.69 | 4.31 |
| 14:30 | 5532 | Wolverhampton vs Liverpool | 5.79 | 4.63 | 1.51 |
| 15:00 | 1034 | Abha vs Al-Ettifaq | 4.82 | 3.93 | 1.64 |
| 15:00 | 1341 | Nzoia United vs Bidco United | 1.93 | 3.20 | 3.70 |
| 15:00 | 2027 | KK Homeboyz vs Tusker | 2.91 | 2.81 | 2.50 |
| 15:00 | 2661 | Athletic Bilbao vs Cadiz CF | 1.55 | 4.01 | 6.38 |
| 15:00 | 4883 | Shabana FC vs Kenya Police | 4.29 | 3.29 | 1.78 |
| 15:00 | 4894 | Bandari vs Ulinzi Stars | 2.09 | 2.81 | 3.76 |
| 16:00 | 3485 | Golden Arrows vs Stellenbosch | 2.08 | 3.09 | 3.50 |
| 16:00 | 4198 | Juventus vs Lazio | 2.00 | 3.34 | 3.99 |
| 16:30 | 2387 | SC Freiburg vs Borussia Dortmund | 2.99 | 3.74 | 2.23 |
| 16:30 | 2732 | Akhmat Grozny vs FC Krasnodar | 2.72 | 3.34 | 2.36 |
| 16:30 | 2796 | VfL Wolfsburg vs Union Berlin | 2.25 | 3.43 | 3.18 |
| 16:30 | 2967 | RB Leipzig vs Augsburg | 1.26 | 6.41 | 9.92 |
| 16:30 | 3748 | Mainz vs Stuttgart | 2.58 | 3.56 | 2.63 |
| 16:30 | 4229 | FC Koln vs Hoffenheim | 2.25 | 3.70 | 2.98 |
| 16:35 | 2404 | AL Urooba vs Masafi | 2.08 | 3.34 | 3.04 |
| 17:00 | 2840 | Aston Villa vs Crystal Palace | 1.92 | 3.66 | 3.92 |
| 17:00 | 3296 | Shakhtar Donetsk vs FC Obolon Kiev | 1.22 | 5.22 | 9.84 |
| 17:00 | 3544 | Tottenham vs Sheffield Utd | 1.29 | 5.97 | 9.47 |
| 17:00 | 4449 | West Ham vs Manchester City | 5.63 | 4.36 | 1.56 |
| 17:00 | 5042 | Manchester Utd vs Brighton | 2.26 | 3.90 | 2.85 |
| 17:00 | 5548 | Fulham vs Luton Town | 1.69 | 3.86 | 5.04 |
| 17:15 | 2876 | Valencia vs Atletico Madrid | 3.70 | 3.34 | 2.08 |
| 17:30 | 4648 | Rio Ave vs Famalicao | 2.51 | 3.16 | 2.71 |
| 17:30 | 5563 | Feyenoord vs Heerenveen | 1.21 | 6.15 | 9.92 |
| 18:00 | 2692 | AL Hazm vs AL Tai | 2.83 | 3.45 | 2.34 |
| 18:00 | 2879 | Al Raed Club vs Al Nasr Riyadh | 9.44 | 5.67 | 1.27 |
| 18:00 | 4226 | Rennes vs Lille | 2.14 | 3.64 | 3.23 |
| 18:30 | 1515 | Kaizer Chiefs vs Bloemfontein Celtic | 1.82 | 3.23 | 4.31 |
| 19:00 | 5449 | Inter vs AC Milan | 2.24 | 3.39 | 3.24 |
| 19:00 | 5472 | Spartak Moscow vs Sochi | 1.64 | 3.96 | 4.42 |
| 19:30 | 1603 | Newcastle vs Brentford | 1.54 | 4.40 | 5.72 |
| 19:30 | 2117 | VfL Bochum vs Eintracht Frankfurt | 2.93 | 3.60 | 2.32 |
| 19:30 | 3343 | FC Thun vs FC Luzern | 3.42 | 3.77 | 1.81 |
| 19:30 | 3797 | Celta Vigo vs Mallorca | 2.04 | 3.15 | 4.13 |
| 19:45 | 2311 | Vitesse Arnhem vs Waalwick | 1.49 | 4.36 | 5.35 |
| 20:00 | 4798 | Sporting Farense vs Sporting Braga | 4.47 | 3.82 | 1.67 |
| 20:00 | 5222 | Adana Demirspor vs Pendikspor | 1.50 | 4.34 | 5.37 |
| 20:00 | 5249 | Galatasaray vs Samsunspor | 1.35 | 4.95 | 7.01 |
| 20:30 | 4344 | Panetolikos vs Panathinaikos | 7.30 | 3.81 | 1.48 |
| 21:00 | 2585 | Al Ahli Jeddah vs Al Taawon | 1.42 | 4.71 | 6.48 |
| 21:00 | 2618 | PSV Eindhoven vs NEC Nijmegen | 1.15 | 7.12 | 12.86 |
| 21:00 | 3563 | Fortuna Sittard vs FC Volendam | 1.60 | 3.98 | 4.67 |
| 21:15 | 4926 | Baltika Kaliningrad vs Rostov | 2.24 | 3.24 | 2.98 |
| 21:45 | 3297 | Genoa vs Napoli | 5.04 | 3.91 | 1.68 |
| 22:00 | 1405 | Heracles Almelo vs Utrecht | 2.47 | 3.36 | 2.57 |
| 22:00 | 3587 | Lens vs Metz | 1.51 | 4.53 | 5.97 |
| 22:00 | 4387 | Barcelona vs Betis | 1.44 | 4.70 | 6.91 |
| 22:30 | 1814 | FC Vizela vs Benfica | 7.75 | 5.17 | 1.31 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# SERIKALI KUIONGEZEA NGUVU TAIFA STARS

Na Saada Akida

BAADA ya timu ya taifa 'Taifa Stars', kufuzu kushiriki fainali ya Mataifa ya Afrika AFCON mwakani, Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) imepanga kuliongezea nguvu benchi la ufundi la timu hiyo kuelekea kwenye fainali hizo za Ivory Coast zitakazofanyika Januari mwakani.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hamis Mwinjuma 'Mwana FA' alisema wanatarajia kuwa na mpango mkakati wa timu hiyo ya Taifa kuiwekea mazingira ya kufanya vizuri katika michuano hiyo.

Alisema moja ya mikakati yao ni kuangalia uwezakano wa kuongeza nguvu kwenye benchi la ufundi kipindi ambacho timu itakuwa kwenye maandalizi.

"Tumefanikiwa kwenda kucheza Afcon mwakani, tunatakiwa kuandaa mpango mkakati wa timu kwenda kushindana, tutakutana na TFF kwa ajili ya hili lakini pia kuna uwezakano wa kuongeza nguvu kwenye benchi la ufundi kuelekea michuano hiyo," alisema Mwana FA.

Aliongeza kuwa anaamini TFF wataandaa timu kwa ajili ya kwenda kushindana katika mashindano hayo na wachezaji watakaoitwa wataipeperusha vyema bendera ya Tanzania .

Alisema hawataki kumuangusha Rais Samia Suluhu Hassan ambaye anajitoa kumairisha sekta ya michezo.

"Mama (Rais Samia) anataka kuona Sekta ya michezo inakuwa imara hatutaki kumuangusha katika hilo kwa sababu anajitoa kwa kununua kila goli kwa ngazi ya klabu katika michuano ya kimataifa, lakini pia ametoa pesa kwa wachezaji wetu wa timu ya Taifa baada ya kufanikiwa kufuzu Afcon, niwaambie tu pesa zipo na wachezaji watapewa haki yao," alisema Naibu Waziri huyo.



Vijana wakicheza mpira wa Kikapu katika Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam, kama walivyokutwa na mpiga picha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simba, Yanga lazima kieleweke, zipo ugenini kuiheshimisha nchi*

INATOKA UK 24

diano jijini Dar es Salaam.

Kocha huyo alipata ushauri kutoka kwa wadau mbalimbali wa soka nchini Zambia, akiwemo kiungo za zamani wa Simba, Rally Bwalya kuwa kama akitaka kutinga hatua ya makundi ni lazima ahakikishe anashinda kwa mabao mengi nyumbani kwani itakuwa ngumu sana kufunga Simba ikiwa Tanzania.

"Nimewaandaa vijana kuhakikisha kufa na kupona tunaweka mazingira mazuri kupata ushindi mzuri nyumbani, halafu ndiyo tutaangalia tutafanya nini katika mechi ya marudiano," alisema Chipepo.

Michezo ya marudiano inatarajiwa kuchezwa jijini Dar es Salaam kati ya Septemba 29 na 30.

# Michezo

Jumamosi Septemba 16, 2023

Nipashe



Sancho atemwa kikosi cha kwanza United UK. 22




# Simba, Yanga lazima kieleweke, zipo ugenini kuiheshimisha nchi

## ●●● Gamondi asema hatokubali kuishia hatua hii, Robertinho kazi imebaki kwa...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KLABU mbili kubwa nchini, Simba na Yanga leo jioni zitakuwa kwenye viwanja vya ugenini nchi mbili tofauti kusaka tiketi ya kutinga hatua za makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Huku klabu hizo zikisaka ushindi wa ugenini, makocha wa timu hizo kila mmoja ameweka wazi mipango yao.

Wakati Simba ambayo haikucheza hatua ya awali na kuanzia raundi ya kwanza itakuwa Ndola nchini Zambia kuumana na Power Dynamos kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa, Yanga wenyewe walioanzia hatua ya awali watakuwa Kigali, Rwanda kwenye uwanja wa Pele kucheza na Al Merrikh ya Sudan na michezo hiyo yote itaanza muda mmoja, saa 10:00 jioni.

Timu zote hizo ziliondoka nchini Alhamisi kwa matumaini makubwa ya kushinda michezo yao ya awali, kabla ya marudiano Septemba 29.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema pamoja na kwamba mechi itakuwa ngumu, lakini amewapanga vijana wake kucheza vile alivyoawaagiza ili kupata matokeo mazuri ambayo yatawarahisishia kazi katika mechi ya marudiano.

"Haitokuwa kitu kizuri kwetu kuishia hatua hii, tunachotaka ni kutinga makundi ili si tu kuwafanya wanachama na mashabiki wa Yanga wawe na furaha, lakini pia hata wachezaji wakubwa waliosajiliwa kuendelea kuonekana katika mechi kubwa na kujitangaza kimataifa," alisema Gamondi.

**Gamondi alisema wanatambua uwezo wa wapinzani wao,lakini nao kwa sasa wameshakuwa moja ya timu kubwa Afrika, yenye uwezo wa kucheza na kushinda popote.**

"Hatuna tatizo wa Al Merrikh, tunatambua ni klabu kubwa, kongwe na huwa inafanya vizuri kwenye hii michuano huwa inaingia makundi mara kwa mara, ila msimu huu na sisi tunayataka makundi hatutaki kuishia hatua hii ya kwanza ," alisema Gamondi.

Yanga itakuwa inajaribu kutaka kutinga hatua ya makundi kwa mara ya kwanza baada ya miaka 24, ambapo mara ya mwisho ilikuwa ni 1998.

Al Merrikh imechagua kucheza mchezo wake Rwanda kutokana machafuko ya kisiasa yanayoendelea nchini kwao.

Nchini Zambia, Kocha wa Simba, Roberto Oliveira amesema wao kama benchi la ufundi wameshamaliza kazi, kilichobaki ni wachezaji kuonyesha kile walichokubaliana kukifanya leo wakati wakiwa kwenye uwanja wa mazoezi.

Alisema watacheza kwa nidhamu kwani wapo ugenini, wanawaheshimu wapinzani wao, lakini nao wanapaswa kuheshimiwa.

"Tunaanza rasmi Ligi ya Mabingwa Afrika, msimu uliopita tulicheza vizuri sana michuano hii, tunawaheshimu wapinzani wetu lakini nao wanapaswa kutuheshimu, mchezo wa mpira wa miguu una matokeo ya ajabu, lakini kwetu tumejipanga vyema ili kushinda, kwangu mimi soka ni sanaa na si ugomvi, hivyo tutacheza soka la pasi fupi fupi, lakini kwa sababu tuko ugenini itatubidi tuubane uwanja ili kutowapa nafasi wapinzani wetu," alisema kocha huyo.

Alisema moja ya mbinu atakayotumia ni kukaa na mpira kwa sababu ndiyo njia ya kujilinda kuliko kuwaachia wapinzani kutawala.

Kwa upande wa mshambuliaji wa Simba Moses Phiri akizungumza mbele ya waandishi wa habari kwenye mkutano wa jana na waandishi wa habari kabla ya mechi, alisema yeye na wachezaji wenzake wamejiandaa vyema na wana shauku kubwa na mchezo huo.

"Wachezaji wote tuko vizuri na kwangu mimi nafurahi kucheza na timu ambayo nafahamu lugha wanayoiongea, hiyo inaweza kutupa urahisi kidogo," alisema straika huyo ambaye ni raia wa nchini hiyo.

Kocha Mkuu wa Power Dynamos, Mwenya Chipepo amesema wanaiheshimu mno klabu ya Simba kwa sababu ni timu kubwa na wazoefu wa michuano hiyo, lakini anataka kuimaliza mechi nyumbani ili asipate kazi kubwa atakapokuja kucheza mchezo wa maru

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >